# Umoja

Jeffersonville, Indiana, USA
Februari 11, 1962

1 Asante, Ndugu Orman. Bwana awabariki.

Habari za asubuhi, marafiki. Ni vizuri kuwa hapa maskanini tena asubuhi hii. Na nilikuwa nimesimama tu kule nyuma nikisikiliza, wakati nikiingia, na kusikia unabii ukitokea kwa njia ya kunena kwa lugha, pamoja na tafsiri. Nami nikawaambia watu ya kwamba chumba hicho kimejaa pia, kwa hiyo nikasema, "Sijui, sijazungumza na mtu huyu" (Huyo alikuwa ni Ndugu Higginbotham, kama nimempata mtu huyo kwa usahihi.) "Kwa muda mrefu. Imekuwa miezi kadha tangu nimempa mkono." Lakini hilo ndilo hasa ninalozungumzia, yale aliyosema asubuhi ya leo, yale hasa ninayonena. Hakujua. Mimi sikujua jambo hilo mimi mwenyewe mpaka kitambo kidogo tu kilichopita, yale niliyokuwa niende kuyanena. Na ni hivyo tu, yale aliyosema papo hapo. Kwa hiyo tuna furaha kujua ya kwamba tumekusanyika katika Jina la Bwana Yesu, na chini ya mbawa Zake zinazolinda.

2 Sasa, ninaona wengi wamesimama, mahali pamejaa na kusongamana, nasi tunachukia tu kuona jambo hili. Na, mara tuwezapo, tutafanya tofauti hapa, maskani kubwa zaidi. Sasa, ninataka kuripoti kutoka Phoenix upesi tu.

Nilikuwa hapa Jumapili iliyopita usiku na kuzungumza juu ya somo la Ushirika kwa … kabla ya ibada ya ushirika. Ushirika siyo kula mkate, ushirika unamaanisha "kuzungumza na, kujibizana, kuzungumza na mtu fulani."

Na sasa asubuhi ya leo, nikichukua muda mrefu kupita kiasi, mbona, mtu fulani hubadilisha viti pamoja na wale wanaosimama, na itathaminiwa, hebu waketi chini kidogo. Ni—ninaguswa na wakati huu tunaoishi. Ninaguswa sana, sana. Ninapoona mambo yakitendeka ninayoyaona yakitukia, kuna kitu fulani ndani yangu kilichochochewa. Nami ninataka kuchukua wakati wangu na kujaribu kuninii …

3 Ujumbe wa asubuhi ya leo nina nena juu ya somo la Umoja. Nami ni—ninataka kuchukua wakati wangu na kujaribu kuufanya tu kama … kuuweka kikamilifu kabisa nijuavyo. Nami ninatamani maombi yenu kama mlivyokusanyika.

Na sasa nawatakeni mfungue, kama mna Biblia na mnataka kusoma pamoja nami, kwenye mlango wa 1 wa Waebrania, kwanza. Nami ninataka kusoma vifungu vitatu vya kwanza vya sura ya 1 ya Waebrania, na kisha Mwanzo 1:26 na 7, kuunganisha hilo pamoja. Na hakuna mtu anayeweza kusema jambo lolote linalofaa kusema isipokuwa Mungu amsaidie kulisema. Na—na hiyo ni pamoja na Ujumbe asubuhi ya leo, pia, juu ya umoja wa watu na Mungu. Sasa katika Waebrania sura ya 1, tunasoma jambo hili.

> *Mungu, ambaye zamani ... alisema na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,*
>
> *Katika siku hizi za mwisho amenena nasi kwa njia ya … kwa Mwanawe, aliyemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa yeye aliumba ulimwengu;*
>
> *Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake, na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu;*

Na sasa katika Mwanzo, sa—mlango wa 1 na kifungu cha 27, 26 na 27, nilisoma jambo hili.

> *Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; nao watawale juu ya samaki wa baharini, na juu ya ndege wa angani, na juu ya wanyama wa kufugwa, na juu ya nchi yote, na juu ya kila kitu. chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.*
>
> *Kwa hiyo Mungu akamwumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba; mwanamume na mwanamke aliwaumba.*

4 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tunapoomba. Nami nina hakika ya kwamba kuna maombi mengi katika wasikilizaji wa ukubwa huu, kwa hiyo labda tunainua tu mkono wetu kwa Mungu, ambaye ana ombi, na kumruhusu kwa kufanya hivi ya kwamba tuna kitu fulani tunachotaka kuombewa. Mungu na amjalie kila mmoja wenu.

Bwana, tumekusanyika chini ya paa la maskani hii, nasi tunashukuru kuwa na paa juu yetu leo, bali kukusanyika kwetu pamoja kulikuwa kwa kusudi kubwa kuliko hili. Tunajisikia ya kwamba kwa ahadi ya Mungu tumekusanyika chini ya mbawa za Mwenyezi. Kwamba Yeye, kama vile kuku angewafunika vifaranga wake, angetulinda na yote tunayomtaka atulinde nayo. Ili kwamba Yeye aingie juu yetu na kutulisha na atupe leo mkate wetu wa kila siku, kimwili na kiroho, ili tupate nguvu endelevu za mwili kutuwezesha kutembea juu ya nchi, na nguvu za endelevu za Roho Mtakatifu kuleta Neno la Mungu kwa watu wenye njaa. Na kuondoka hapa tukiwa na Hilo midomoni mwetu na mioyoni mwetu, tukiwa na Mafuta mapya ya upako ambayo tungeweza kuwaambia wengine kuhusu siku tunayoishi, na hali ya

wakati. Mungu, tunakutumainia kabisa. Hakuna mahali pengine paliposalia ambapo hakuna mtu angeweza kwenda. Tunajisikia kama Petro alivyojisikia, siku ile Yesu aliposema, "Je! Ninyi pia mtakwenda?"

Yeye alisema, "Bwana, tungeenda wapi? Wewe peke yako unayo Maneno ya Uzima wa Milele." Na hiyo ndiyo sababu tunakusanyika katika Jina Lako asubuhi ya leo, kwa sababu Wewe peke Yako una Maneno ya Uzima wa Milele. Nasi tunaomba ya kwamba utalifanya jambo hili kuwa halisi sana kwa kila mmoja wetu leo hivi kwamba mioyo yetu itawaka moto ndani yetu. Nafsi zetu zitaimarishwa, miili yetu itaponywa, roho zetu zitaponywa, nafsi zetu zitafanywa upya, zimeumbwa kwa mtindo ambao Mungu angetutaka.

5 Baba, ninaomba ya kwamba utawapa nguvu wale wanaosimama kwenye vyumba na kuzunguka kuta, na kwenye korido. Ninaomba ya kwamba utawapa nguvu. Na, nikijua hili likienda kwenye kanda, hilo litaenda kwenye mataifa mengi mbalimbali, huko nje katika nchi na makabila ya dunia. Na, Mungu, tunakutumaini Wewe kabisa. Tupe tu nguvu na Neno—Neno na upako, kusudi iwe hivyo tu unavyoweza kufanya kwa ajili ya saa hii. Tunajikabidhi Kwako sasa, kusikiliza kwetu, sauti yetu, usikivu wetu, yote tuliyo, tunayakabidhi Kwako, kwamba Wewe utatenda kazi ndani yetu. Fanya kazi kupitia kwetu na udhihirishe Uwepo Wako mkuu pamoja nasi. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao. Amina.

6 Neno umoja linamaanisha "kuwa mmoja pamoja." Umoja, "lioungana." Na, sasa, hili ni somo kabisa, na lina—linastahili kuangaliwa sana kuliko ninavyoweza kulitoa, na zaidi ya vile mtu ye yote duniani angeweza kutoa. Lakini ningependa kuwaeleza maoni yangu juu ya hilo, na, kwa yale Mungu atakayotupa. Sasa, katika hili, ni kufundisha mafundisho. Na kwa ndugu ambao wanaweza kuisikia kanda hii, ninatumaini ya kwamba haitakuwa ni kosa, bali itakuwa ni kukufanya uchukue jambo hili kwa makini sana, zaidi ya hayo. Kwamba ungeisoma kwa maombi, kwa uangalifu, na kuipima katika mizani ya Neno la Mungu, kuona kama ni la Mungu ama la.

Kwa kuwa ninaamini ya kwamba hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya daima, kupima mambo kwa Neno, kwa sababu Neno ndilo Kitu pekee kitakachoweza kudumu. Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita." Hiyo ndiyo sababu ninaliamini, na kuliamini kuwa ni mpango wa Mungu. Ninaamini ya kwamba Hiyo ndiyo kazi iliyomalizika ya Mungu iliyoandikwa katika Neno. Kwa hiyo, kwamba kama kitu chochote kingekuwa kinyume cha Neno hilo, haingeweza kuwa ni Mungu wala mpango wa Mungu. Ninaamini ni mpango. Sasa, Roho wa Mungu katika Neno hulifanya Neno liishi Lenyewe, litende lenyewe. Linalihuisha Neno, kama mbegu.

7 Sasa, mwanamume wa kwanza na mwanamke wa kwanza katika Bustani ya Edeni walikuwa katika upatano mkamilifu na Mungu, kiasi kwamba Mungu angeweza kushuka chini wakati wo wote aliotaka na kuzungumza na Adamu na Hawa mdomo kwa sikio. Sasa, huo ni umoja mkamilifu, Mungu na uumbaji Wake, Mungu akinena mdomo kwa sikio na Adamu na Hawa. Nao walikuwa wakamilifu sana katika upatano na Mungu hata wakawa mmoja na Mungu. Mungu na familia Yake walikuwa mmoja.

Mtu ye yote na familia yake, familia sahihi, nzuri, ya heshima, tiifu ni imeunganika na nyingine, familia yoyote. Na kama kuna jambo fulani katika familia ambalo linawatenganisha, basi si sawa, familia imevunjika mahali fulani. Yawapasa wote wawe mmoja, baba pamoja na mama, mama na baba, watoto na mzazi, mzazi na watoto, wote wakikubaliana. Na, unapoona jambo hilo, utaona picha moja nzuri.

8 Hilo ndilo kusudi la Mungu. Na kusudi Lake kama Baba, aliye mkuu, lilikuwa ni kuwa mmoja na familia Yake, familia ya duniani, Adamu na Hawa. Na njia pekee ambayo wangeweza kuwa mmoja na familia, ama na Mungu, ilikuwa ni kwa sababu asili ya Mungu ilikuwa ndani yao. Kwa hiyo iliwafanya kuwa na tabia ya Mungu ndani yao, halafu wao kwa wao na kwa Mungu, wote wakawa mmoja. Hiyo si ni picha nzuri, Mungu katika familia Yake, Baba juu ya wote, aliye mkuu! Hakuna mauti, hakuna huzuni, hakuna maumivu ya moyo, hakuna kitu; furaha tu isiyoelezeka; wasiwe wagonjwa kamwe, wasiwe na maumivu ya moyo, mmoja tu pamoja na Mungu! Ni picha iliyoje! Kwa sababu, asili halisi ya Mungu ilikuwa ndani ya watu hawa. Na kwa hiyo, yale waliyofanya, walifuata tu sawa na Mungu, na Mungu pamoja nao akawafanya mmoja.

9 Sasa, Yesu aliomba, katika Yohana, mlango wa 17 na kifungu cha 11, kwenu ninyi mlioandika maandiko haya ya shule ya Jumapili. Nina mengi yao asubuhi ya leo. Yohana 17:11, Yesu aliomba ya kwamba Kanisa na Yeye wangekuwa mmoja kama Yeye na Baba walivyokuwa mmoja. Ili kwamba Kanisa, sisi kama washiriki wa Mwili wa Kristo, tungekuwa mmoja, pamoja, kama tu Yeye na Baba walivyo mmoja. Na siku hiyo tungejua ya kwamba Yeye alikuwa ndani ya Baba … Baba ndani Yake, na Yeye ndani yetu, ya kwamba pamoja tulikuwa mmoja. Ni muungano wa jinsi gani, umoja ambao ungekuwa, kumwona Mungu katika Kanisa Lake mpaka kila mshiriki anapatana kabisa na mwingine na Mungu. Hilo ndilo Kanisa aambalo Yesu anakuja kwa ajili yake. Hapo ndipo maombi Yake yatakapojibiwa, kwamba tutakuwa mmoja.

10 Na ndiyo msingi pekee wa ushirika ambayo Mungu amewahi kuweka kwa ajili Yake Mwenyewe na Kanisa Lake, ni umoja Wake Mwenyewe katika watu. Huo ndio msingi pekee wa ushirika. Na njia pekee unayoweza kuwa na misingi hiyo ni kwa muungano, kuunganishwa Naye milele. Kama tu vile unapoungana na mume wako, mwanamke kuungana na mumewe, ni nadhiri mpaka mauti. Sasa, basi unapoungana na

Mungu, ni jambo lile lile ambalo kanisa liliungana na Kristo, ni mpaka mauti tunatengana. Na halafu kama hutatenda dhambi wala kufanya jambo lo lote baya, utaunganishwa Milele na Mungu. Na ni mauti tu yanayoweza kukuondoa kwa Mungu, na si mauti ya kimwili, bali dhambi ya mauti. Dhambi ni mauti, na hiyo inakuondoa kwa Mungu. Kwa hiyo, kuunganishwa Naye katika Roho wa nguvu Zake, ni Uzima wa Milele, umeunganishwa Milele na Mungu. Loo, ninataka kufikia jambo hilo baada ya kitambo kidogo. Wameungana Milele na Mungu wa Milele, wakiwa katika upatano mkamilifu Naye, wameungana pamoja kikamilifu, Kanisa ambalo wote, wote wawili Mungu na Kanisa Lake, ni mmoja, wameungana pamoja.

11 Na kama utaona jinsi ambavyo Hawa aliungana na Adamu, yeye akawa sehemu yake. Mungu, je! Uliona katika Mwanzo 1:27, Yeye alimuumba mwanamume na mwanamke, aliwaumba. Sasa, huyo mwanamume alikuwa … wa kiume na wa kike alipofikia kuwa katika roho ya kike na ya kiume. Ndipo Mungu akachukua ubavuni mwake ... ubavu. Je! Uliona sehemu ya mwili ilikuwa zao la kitu fulani, bali si roho? Sehemu ya mwili wa mwanamke ilikuwa ni zao la kitu, baada ya uumbaji kukamilika, Mungu alichukua ubavuni mwa Adamu ubavu na akamfanya mwanamke. Lakini si roho, huyo roho alikuwa ni sehemu ya Adamu, kwa maana yeye alikuwa mwanamume na mwanamke pia, mwanam … akinena kiroho, wa kiume na wa kike pamoja.

12 Sasa, hivi hamwoni ile picha kuu? Sisi, katika mwili, wao ni tofauti. Sisi ni kama kitu zao la kitu kingine, kiumbe kilichoumbwa, kwa ndoa takatifu. Lakini katika Roho sisi ni wana na binti, si roho mwingine, bali Roho wa Mungu aliye hai. Sisi tuko katika mfano Wake, katika umoja Wake, katika sura kamilifu ya Mungu aliye hai, kwa sababu tumekuwa wana na binti. Si waliotengwa, bali ni Roho yule yule, Mungu yeye yule, Mtu yule yule, aliyeunganishwa katika ndoa ya Milele. Ona jinsi Mungu alivyopanga jambo hilo kwamba hatupaswi kuwa tofauti, bali Yeye! Sio kiumbe kingine cha kabila lingine, bali muungano halisi na uzao wa Mwenyezi, uliofanywa na muungano mtakatifu. Sasa, mwili unatoka kwa mama na baba, bali Roho hutoka kwa Mungu, Mungu akijitenga Mwenyewe kama vile Adamu alivyotenganishwa.

13 Kwenye Siku ya Pentekoste, tunamwona Roho Mtakatifu, ile Nguzo ya Moto, ikijitenga na kuketi juu ya kila mshiriki wa Kanisa hilo, Mungu akijiweka mwenyewe pamoja! Halafu pamoja na kundi hilo la watu pamoja, linafanya nini? Huurudisha Mwili ulioungana wa Bwana Yesu. Tukija pamoja!

Na leo katika utengano huu mkuu tunaoishi ndani yake, tofauti za kimadhehebu na kadhalika, ni huzuni jinsi gani, ni aibu jinsi gani!

14 Tuliunganishwa na ndoa ya Mbinguni na Mungu wa Milele, sehemu Yake, sehemu ya Mungu. Katika mwili ninakuwa Branham kwa sababu ya baba yangu, Branham. Unakuwa sehemu ya baba yako na mama yako, lakini katika roho tunakuwa katika umoja na Mungu, ni sehemu ya Mungu. Hiyo ndiyo sababu roho haiwezi kufa. "Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa milele. Na katika mfano kwamba yeye yuko hapa duniani, na katika sura yake, nitamfufua katika siku za mwisho." Si kiumbe cha kiroho, kwa kuwa tutakuwa na mwili kama Mwili wenye utukufu wa Mungu, Mwili uliotukuzwa wa Bwana Yesu, ulioinuliwa katika Mfano Huo.

15 Yesu alisema, akienda kwenye kaburi la Lazaro, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, ataishi. Na kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Aniaminiye Mimi, si juu Yangu, bali ndani Yangu." Kuwa ndani Yake, tukiamini! "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu ndani yenu." Ndani Yake, tukiamini! Loo, jamani! Natumaini Roho Mtakatifu atashusha jambo hilo moja kwa moja kwenu. Sasa, ninyi ni kundi dogo, hiyo ndiyo sababu kupitia juma hili, nikiomba na kumwomba Mungu, nilichagua somo hili, kuwaonyesha mahali tunaposimama. Kumwamini Yeye. Huwezi kumwamini mpaka utakapokuja ndani Yake, ama, Yeye anakuja ndani yako, ndipo unamwamini, ndipo una Uzima wa Milele. Unamwamini mpaka utakapopata Uzima wa Milele, ndipo Uzima wa Milele ni Uzima wa Mungu ndani yako, ndipo unamwamini.

"Ninyi ndani Yangu, Mimi ndani yenu. Ili kwamba waweze kuwa mmoja, Baba, kama vile Wewe na Mimi tulivyo mmoja." Mungu katika Kristo, Kristo katika Kanisa. Unaona? "Kama tu vile tulivyo mmoja, vivyo hivyo wao wawe mmoja." Basi unawezaje kuwa mmoja? "Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu ndani yenu." Mnaona, kaeni! "Maneno Yangu ndani yenu, basi ombeni mtakalo." Kwa kuwa si wewe tena, ni Neno lililo ndani yako, nalo Neno ni Mungu.

16 Sasa, Neno la Mungu ni Upanga. Waebrania, mlango wa 4, inasema hivyo, Waebrania 4:12. Sasa, ni Upanga. Na upanga umetulia kikamilifu kama hautolewi kwa mkono wala nguvu. Nao … lakini inahitaji mkono kushikilia Upanga. Na chukua mkono unaoshikilia Upanga huu, ni mkono wa imani.

Sasa, huo mkono wa imani, inategemea una nguvu jinsi gani. Mkono huu wa imani huenda ukawa na nguvu za kutosha kukata shimo dogo kwenye giza na kusema, "Kwa imani nimeokolewa." Huo ni mkato mzuri sana, lakini, basi, kama huzo ndizo nguzo zote huo mkono unaweza kushikilia Upanga huo, hivyo tu ndivyo unavyoweza kukata. Lakini, kama ni mkono wenye nguvu, utakata kila kitu ambacho Ibilisi anaweza kuweka huko nje, kufanya kila ahadi ya Mungu iangaze katika nguvu za kufufuka Kwake. Kama ni mkono wenye nguvu wa imani, "Siku za miujiza! Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele," ilikata

njia yake moja kwa moja. Inategemea nguvu za mkono nyuma ya Upanga.

17 Na Upanga ni mkali sana. Waebrania 4, ilisema, "Ni kali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili unaokata na kuondoka, na hata kwenda kwenye—kwenye mafuta ya mfupa, na kwenye viungo, na huyatambua mawazo ya moyo." Likienda zaidi ya la kimwili, linaingia katika miliki ya kiroho na kuyachukua mawazo ya moyo na kuyafunua. Roho wa Mungu, Neno la Mungu.

Sasa, Neno hilo litakata mle ndani kama kuna mkono wa kutosha nyuma Yake kulisukuma ndani, litapata mahali Pake na kukata kila ahadi na kukupa, kama tu una mkono wa kutosha nyuma Yake. Upanga, uuchukue katika mkono—mkono wa imani! Ushike vizuri, ushikilie na uingie katika uso wa adui. Adui huyo asiyetahiriwa anawezaje kusimama katika Uwepo wa Mungu wa Milele? Kwa hiyo, chukua Upanga wa Neno, na kila ahadi ni yako. Uchukue katika mkono wenye nguvu wa imani, tembea mbele! Kama unahitaji uponyaji, ukate kwa Neno, "Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele." Kama unahitaji wokovu, kila ahadi katika Biblia ni yako. Liko nyuma kule ndani na Shetani anajaribu kulificha, bali chukua Upanga na usukume kupitia gizani mpaka Nuru ya Mungu iangazie nafsi yako na uwe na ahadi. Yeye atalifanya hilo.

18 Adamu alikuwa sehemu ya, ama, Hawa alikuwa sehemu ya Adamu, yeye alikuwa nyama ya nyama yake na mfupa wa mfupa wake. Na hivyo ndivyo muungano sahihi ulivyo. Na hivyo ndivyo muungano sahihi wa Kanisa ulivyo, Roho wa Roho Wake, Neno la Maneno Yake. Kamwe hajaliacha Neno, mwamini halisi wa kweli hatapatana juu ya Neno lo lote. Kumbukeni, ilikuwa ni Neno moja tu ambalo Hawa alipatana juu yake, Neno moja. Bali mwamini wa kweli hatapatana juu ya Neno lo lote. Utashikilia Upanga wa Imani kwa … katika imani, hasa, Upanga wa Neno, na kudai kila ahadi ya Kiungu ambayo Mungu alifanya. Hivyo ndivyo ilivyo.

19 Walikuwa ni mifano ya Mungu kwetu, jinsi tunavyopaswa kuwa, wao, kuwapo daima, wasioshindwa kamwe. Walipozungumza, Mungu alijibu. Aliwaangalia, kila siku. Usiku, walipokuwa wamelala, Yeye aliwalinda. Mchana, Yeye aliwaongoza, akawalisha, akawapenda, akafanya ushirika nao daima, wakati wote. Walikuwa katika mfano wa Mungu, na Mungu alikuwa ndani yao. Hilo ndilo linalofanya ushirika. Hilo ndilo linalounda muungano, ni Mungu katika Kanisa Lake. Huo ndio muungano. Mengi yangeweza kusemwa, ana sehemu nyingi za kwenda. Ukiungana Naye, ni Uzima wa Milele. Na njia pekee tunayoweza kuungana Naye ni kuja kila nukta ya Neno Lake. Hiyo ni kweli, chukua kila ahadi na uiamini.

20 Sasa, Hawa aliunganishwa mpaka alipovunja Neno moja, ama, akatilia shaka Neno moja kuwa ni kweli. Hilo lilimtenganisha. Kila Neno, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno!" Kwa hiyo tunaweza kuwa katika Mungu, tumeunganishwa, kwa sababu Adamu na Hawa, kabla ya anguko, kabla ya kutokuamini Neno, ilikuwa ni mfano wa kile tungeweza kuwa ndani Yake. Kuunganishwa Naye, ni Uzima; kutengwa Naye, ni mauti. Sasa, kama tukifuata amri Zake!

21 Tunajua tunafanya makosa, bali huna budi kuangalia hilo. Si makosa yako, kwa sababu daima utayapata. Lakini, unaona, ni kufuata Kanuni Zake, kufuata yale aliyosema ufanye. Kujikwaa na kuanguka hakuhusiani na jambo Hilo. Mtumishi halisi wa kweli, kama atajikwaa, atasimama tena. Kama akiyumba, Mungu humvuta moja kwa moja kwenye njia, mradi tu yuko kwenye njia ya wajibu. Lakini kama yuko nje ya wajibu, Mungu hawajibiki kwake. Lakini mradi tu yuko kazini, Mungu anawajibika kwake, akijua ya kwamba yeye ni mwanamume tu ama mwanamke. Yeye anawajibika kwa mtu huyo mradi tu wako kwenye wajibu.

22 Sasa, Kanisa sasa limeposwa na Kristo kwa ajili ya arusi. Arusi haijapata kufanywa bado, itakuwa kwenye Karamu ya Arusi ya Mwana -Kondoo. Kwa hiyo, tunaona ya kwamba Kanisa sasa limechumbiwa, kama vile mwanamume alieposwa kwa mkewe. Yeye anafanya nini wakati wameposana? Yeye anampa tu kila namna ya vitu, anamtumia zawadi, anamfanya ajisikie vizuri. Vema, hivyo ndivyo Kristo anavyolifanyia Kanisa Lake. Yeye anatutumia karama za Roho. Unawezaje kuposwa basi wakati unakana karama hizi? Ni ishara halisi za upendo. Ni ishara ya Mungu kwa Kanisa. Yesu alisema hivyo, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

23 Sasa, weka mambo hayo akilini. Kanisa halina budi kuamini kila Neno, kila ahadi, kila kitu, na kulidai kwa ajili yao wenyewe, na kufanya mazoezi ndani Yake. Kama nilikuwa nimeposwa na msichana, nami nilikuwa mseja, nami ningemtumia kitu fulani, pete ya posa, naye asingeivaa, basi hiyo inaonyesha yeye haniamini. Yeye—yeye—yeye hataki kuwa bibi -arusi wangu. Na kama Kristo analipelekea kanisa Lake karama alizoahidi, nao wanazikataa na kusema "haziko hivyo," hawataki kuwa Bibi -arusi wa Kristo. Wao wameposwa na mpenzi mwingine, na si kwa Kristo, Bwana Arusi. Kwa hiyo Kanisa halisi hutimiza ahadi, na kutimiza yote, na kukubali karama ambazo Mungu huwatumia. Vema.

24 Sasa, wanadamu wa kwanza walijitenga na ushirika wasimwamini Mungu, kwa kutokuamini Neno Lake na kusikiliza uongo wa ibilisi. Sasa, hicho ndicho kitu cha kwanza kilichoondosha ushirika huu wa ajabu. Sasa angalia, Adamu na Hawa wakiwa katika hali ya kutokufa kamwe, katika hali ya kutokuwa wazee, wasiwe wagonjwa kamwe, wasiwe na wasiwasi kamwe.

Unasema, "Hakika ningetamani ningekuwa hivyo." Hebu ni- … Nina habari kwa ajili yenu, mko katika hali ile ile. Mungu huweka jambo hilo kwa kila kiumbe duniani, katika mahali pale pale.

25 Makubaliano yalikuwa nini? "Kama mtayashika Maneno Yangu! Kama, Neno Langu, kama utalitimiza, unaliamini na kulitekeleza!" Lakini mara ya kwanza kabisa ambayo Hawa hakuamini, aliondoa Neno moja kutoka kwa yale Mungu aliyosema, lilivunja ushirika na ule muungano mkuu. Na wakati ambapo kanisa liliacha kuamini Neno lo lote la Biblia ya Mungu, na kuliweka mahali pengine, ndipo wanavunja ushirika huo wa ajabu ambao walipewa, na kuwa waliotengwa. Mara alipofanya jambo hilo, mauti ikaingia katika mwili wake unaopatikana na mauti. Sio tu mwili wake unaokufa, bali na hali yake ya kiroho. Alivunja uhusiano na Mungu, dakika tu alipoacha kuamini. Na hakuna mtu anayeweza kuamini … Hili hapa! Hakuna mwanamume, hakuna mwanamke anayeweza—anayeweza kuamini uongo wa ibilisi mpaka hawajaamini Kweli ya Mungu. Hakuna mtu anayeweza kuamini uongo wa ibilisi mpaka hawajaamini Kweli ya Mungu. Kwa hiyo, unaona, Hawa, Adamu, ambapo inatuweka asubuhi ya leo.

26 Sasa hebu na tufikirie kwa uzito, kwa sababu hatutaweza kuwazia tena baada ya jambo hili, baada ya maisha haya ya kibinadamu kwisha. Mawazo yako ndiyo sasa. Huwezi kuchagua baada ya jambo hili, huna budi kuchagua sasa, kwa maana hii ndiyo siku ya kuchagua, kufanya chaguo lako. Sasa yeye, Neno moja, si Amri kumi zote, Neno moja tu, alimhoji Mungu kwa sababu aliwasilishwa kwake katika nuru hiyo, ya kwamba Neno hilo lilikuwa linatia shaka. Neno la Mungu haliwezi kutiliwa shaka, alimaanisha tu kile alichosema. Lakini yeye alihoji kwa sababu liliwasilishwa kwake, "Loo, hakika Mungu hakumaanisha jambo hilo." Lakini Yeye alimaanisha jambo hilo! Mungu humaanisha kila Neno asemalo. Wala halhitaji tafsiri yo yote ya kibinafsi, ni jinsi tu alivyosema.

Vema, tuseme, "Jinsi unavyojua kuhusu Biblia." Ninaamini ya kwamba Mungu wangu ameiongoza Biblia hii, Yeye hulilinda Neno Lake. Yeye alijua ya kwamba wasioamini Mungu na makafiri wangefufuka katika siku za mwisho, kwa hiyo Yeye anailinda. Hivi ndivyo hasa Mungu alivyolikusudia. Ndivyo ilivyo kwetu sasa. Sasa hatuna budi kuliamini. Neno moja kutoka Kwake, nasi tunapoteza ushirika wetu, tunaenda hadi—mautini, kujitenga Milele na Mungu, kama tu vile Adamu na Hawa walivyofanya. Hatuna budi kuamini Kweli ya Mungu.

27 Hebu nifanye hivyo tena. Usikose kuamini Neno lo lote la Biblia ya Mungu. Lakini usiseme tu, "Naam, ninaamini." Sema "lakini"? La, hakuna kitu kuhusu hilo. Unaliamini, utalikubali. Kama ukiliweka kando, ukisema, "Vema, kanisa langu haliliamini hivyo," basi huamini kwamba ni Neno la Mungu, nawe utaondoka chini ya hukumu ile ile ambayo Hawa alienda chini yake. Ulijitenga na wa Milele wakati ulipopata nafasi ya kuungana Naye. Sasa, kumbukeni, Hilo haliwezi kuhojiwa, kwa sababu lilikuwa ni Neno moja, hilo, katika Neno la Mungu.

28 Na, sasa, kama Mungu alikuwatu—na Maneno machache ambapo watu hawana budi kutii, na katika Maneno hayo machache mmoja wapo liliwasilishwa vibaya, likasababisha mauti, angalia Maneno tuliyo nayo leo! Unaona? Inatupasa kupokea kila moja ya hayo, kuyashikilia na kuyaingiza kama ahadi kutoka kwa Mungu. Na mke wa kweli wa Mungu atafanya jambo hilo, mchumba wa kweli aliyeposwa. Sasa, natumaini mambo haya madogo yataingia kwenye kilindi sasa ili tuweze kuyashika.

29 Ni kitu gani cha kwanza kilichomfanya Hawa kutokuamini Neno la Mungu? Ilikuwa ni kwa sababu Shetani alimwahidi hekima zaidi, "Utakuwa na hekima." Sasa, unaona, jamii ya binadamu daima inatafuta kitu fulani. Naye Hawa alikuwa akitafuta hekima zaidi.

Sasa hebu na tusimame kwa dakika moja tu. Hiyo si ndiyo hali ya ulimwengu siku hizi? Wanataka hekima zaidi, tabaka bora, wenye elimu ya juu, wakitaka kitu kilicho tofauti, hekima zaidi. Hicho ndicho Hawa alichotaka. Lakini hebu niseme jambo hili pia, ya kwamba hakuna hekima inayoweza kushinda hekima ya Mungu, hata hivyo ni katika hali ya unyenyekevu sana hivi kwamba watu wanalikosa.

Shetani, kama nilivyosema mara nyingi, yeye hung;aa, bali Injili humeka. Loo, kuna tofauti kabisa kati ya kung'aa na kumeka. Hollywood inang'aa, bali Kanisa linawaka kwa nguvu na upendo wa Mungu. Hollywood inang'aa. Ni tofauti kabisa kati ya kumeka na kung'aa. Hatutaki kung'aa. Tunataka kumeka.

30 Leo, ni vibaya sana kuwazia jambo hili, bali makanisa yanajaribu kutegemea ufahamu wao wenyewe, kama tu vile Hawa alivyofanya. Aliwazia, kwa sababu iliwasilishwa kwake, lilionekana halisi sana. Loo, msikose kulipata hili. Ilionekana halisi sana, kitu ambacho kingeweza kuongezwa kwa yale Mungu aliyosema. Ilionekana kana kwamba angekuwa na kitu ambacho Mungu hakumwambia ni umbali gani angeweza kwenda. Mungu hakuwa amempa mpaka kama vile Yeye alivyoweka bahari na haiwezi kupita kwa sababu mwezi huiangalia. Aliwazia … Alidhani ya kwamba Shetani alikuwa na kitu fulani kwenye mpira, kama tunavyosema, kwamba angali anaweza kuwa katika muungano na Mungu, na hata hivyo awe mwerevu, angekuwa na elimu bora zaidi. Lakini Mungu alikuwa amemkabidhi kile hasa alichohitaji.

Naye amelipa kanisa jambo lile lile. Huko si kujisokota kwa seminari, ama kuingia ama kujisokota kutoka kwenye—kwenye shule ya Biblia. Lakini ni kile hasa kilichoandikwa, na BWANA ASEMA HIVI! Haiwezi kubadilisha hilo! Lakini makanisa yanaegemea ufahamu wao wenyewe. Wao—wao wanafikiri labda

ni ninii … kuna jambo fulani ambalo wamewekewa, na linadanganya.

31 Sina budi kungojea tu hapa kwa dakika moja. Ulimwengu mzima unategemea jambo hilo. Uchumi wote wa taifa hili unategemea mawazo ya uongo. Nikwambie utani mdogo juu yangu mwenyewe, si utani; bali unajua sisi sote tunawapenda wake zetu, ama, tunapaswa. Nami nilikuwa nikiangalia kipindi fulani hapa wakati fulani uliopita huko Magharibi, kimekuwa muda mrefu uliopita, yapata miaka mitatu. Na katika chumba changu asubuhi moja niliamka, na kulikuwa na televisheni chumbani. Nami nikawaza, "Inaonekana kama hali ya hewa ni mbaya." Nami nikawazia, "Vema, saa mbili kamili inawapasa kutoa habari." Nami nikapata kijitabu kidogo cha maelekezo, kilisema habari fulani wakati fulani.

Nikawasha habari, na wakati nilipokuwa nikisikia habari hiyo, ndipo nikaona kwamba katikati ya matangazo ya habari walianza kutangaza aina fulani ya bidhaa, aina fulani ya sabuni. Kisha akasema, "Haikubidi kuosha vyombo vyako tena, mama. Jambo pekee unalofanya ni kutumbukiza moja kwa moja majini na kukiacha kiketi pale kwa dakika kadhaa, kukinyanyua moja kwa moja na kukiweka kwenye ubao wa kutoa maji, yote yamekwisha."

Nikawaza, "Nitakuwa shujaa nitakapofika nyumbani." Niliandika jina lake, hiki kitu fulani. Nikasema, "Nitamwambia mke wangu, 'Angalia kile ninachoweza kufanya!'"

Kwa hiyo nikaenda nikachukua chupa ya kitu hiki na hiki, nami nikakinyunyiza chote majini. Nilimwambia aendelee kufagia nyumba, ningerekebisha hilo kwa ajili yake. Kwa hiyo nikachukua sahani za watoto na kuziondoa makombo, na kadhalika, na yai likang'ang'a juu yake, na kuliangusha chini majini na kuliacha liketi kwa dakika chache, na kuvitoa na kuviweka pale. Kulikuwa na yai la kutosha tu juu yake kama ilivyokuwa wakati nilipoweka mle ndani. Unaona, ni—ningepoteza … Mke wangu angepoteza imani nami wakati huo.

32 Mnaona, kwa nini taifa, kwa nini hawa … taifa hili linawaacha watu wadanganywe? Hilo halipaswi kuruhusiwa kusemwa hivyo. Hilo linapaswa kuwa ni kinyume cha sheria. Kuhusu tangazo la kisasa la sigara, ni aibu iliyoje, "Si kikohozi kwenye lori," kila namna ya. Hilo halipaswi kuruhusiwa. Inafanya nini? Ni kudanganya. Kuna mauti katika kila mmoja wao. Kuna mauti katika kunywa wiski; ubakaji, mauaji, kichaa, kwenye chupa. Lakini hata hivyo tunaruhusiwa kuiweka kwenye vipindi vyetu na kuitangaza kama "Ile aina ambayo babu alikunywa. Furaha zaidi kutoka maishani," aina fulani za vinywaji vya bia na pombe. Ni kitu gani? Ni kudanganya. Ni kuweka kitu fulani mbele ya umma wajiue nacho. Nasi tunaruhusiwa kufanya hivyo.

33 Na hebu nigeuze hilo moja kwa moja. Na makanisa kwa njia ya mafundisho ya sharti ya kujibunia, kanuni za imani za kujitengenezea wanatoa wokovu mkuu kwa watu, nao wanaangukia jambo hilo, ambalo ni mauti. Hakuna kanisa litakalosafisha nafsi yako. Hakuna kanuni ya imani inayoweza kuisafisha nafsi yako. Ni Damu ya Yesu Kristo tu inayoweza kuisafisha nafsi yako, dawa ya Mungu, inaungwa mkono. Kwa hiyo ni uongo tu, bali watu hutegemea ufahamu wa wenye hekima, nao wanakufa kwa huo. Na watu siku hizi wanategemea ufahamu wa—wa kanuni za imani na madhehebu, na mamilioni kama nguruwe waliochinjwa wanaingia kwenye shimo la kuzimu. Ni aibu iliyoje. Tumekatazwa kutegemea akili zetu wenyewe. Hatuwezi kujaribu.

34 Unasema, "Hivi halmashauri ya mwanadamu haikupaswa kusema mengi juu Yake kuliko mtu mmoja?" Sio kama mtu huyo mmoja anasema Neno la Mungu. Kulikuwako na manabii mia nne wakati mmoja waliokuja mbele ya wafalme wawili, nao wakazitegemea akili zao wenyewe. Lakini kulikuwa na mmoja ambaye alidumu na Neno la Mungu na ikathibitisha kwamba alikuwa sahihi, Mikaya. Inategemea kama ni Neno la Mungu. Chochote kinyume cha Neno ni kosa, kinakuja katika mauti. Hakuna hekima inayoweza kupita hekima ya Mungu. Yeye ndiye mwerevu kuliko wote. Yeye ni—Yeye ni Chemchemi. Yeye ndiye chanzo pekee cha hekima. Kila neno la mwanadamu ni upumbavu na uongo, bali ni la Mungu, kama ni kinyume cha Mungu. Sasa, kama mtu huyo anasema Neno la Mungu, basi si—si neno la mwanadamu tena, ni Neno la Mungu. Unaona, si ufahamu wa mtu huyo.

35 Shetani atakufanyia kila namna ya ahadi, bali hana kitu cha kukupa, kwa sababu hana kitu. Hana wokovu wowote. Shetani ni nini? Chochote kinyume cha Neno. Yeye hana wokovu, hana Nuru. Ufalme wake ni giza, mwisho wake ni mauti. Giza na mauti ni ufalme wa Shetani. "Ndugu Branham, rudia tena. Ufalme wa Shetani ni nini?" Chochote kinyume cha Neno la Mungu.

Sasa, huko ni kukata, bali ni wakati wa kukata. Unaona? Tawi, mti, kama utazaa, hauna budi kupogolewa. Ni wakati.

Cho chote kinyume cha maagizo ya Mungu, Neno la Mungu, si Mungu. Ni kitu gani, dhambi ni nini? Haki iliyopotoshwa. Mauti ni nini? Maisha yaliyopotoshwa. Ufalme wa Shetani ni nini? Chochote kinachoweka kitu fulani kuchukua mahali pa Neno, cho chote, mafundisho yoyote. Neno moja, neno moja tu. Huenda ukaamini kila sehemu, Hawa aliamini kila sehemu Yake kwa Neno hilo moja. Hilo Neno moja ndilo tu alilohitaji kutokuamini. Hilo Neno moja ndilo tu unalohitaji kutokuamini.

36 Sasa hebu na tuliangalie. Njia pekee ya kukaa katika ushirika wa Kiungu, ilikuwa ni kulishika Neno hilo. Mungu alisema, "Utafanye jambo hili. Usifanye jambo hili. Utafanya hivi, nawe unaweza kufanya hivi na kufanya hivi. Lakini usifanye hivi." Sasa, sehemu moja tu ndogo ya amri ambayo yeye hakuitii, na akaanzisha jambo hilo lote. Kwa sababu alifanya jambo hilo, alimfanya kila mtoto mwenye njaa aliyewahi kuwa ulimwenguni, kila maumivu ya mauti, kila huzuni, kila maumivu ya moyo. Alifanya jambo hilo papo hapo. Ni jambo la kuchukiza jinsi gani, kutokuamini Neno la Mungu. Kila mtu anayeugua katika maumivu ya kila mauti yaliyowahi kuwako ama yatakayokuwako, yeye alifanya jambo hilo papo hapo. Kila mtoto mdogo asiyeolewa, alifanya hivyo papo hapo, kila mtoto aliyezaliwa chini ya … nje ya ndoa. Kila dhambi iliyowahi kufanywa, aliisababisha papo hapo kwa kuweka kila Neno moja kwa moja ila mahali pamoja padogo hapa. Yeye—yeye alihoji. Yeye alininii tu … Yeye hakulipuuza. Yeye alijua jambo hilo, bali yeye tu … Yeye alishawishika kufanya jambo fulani bora zaidi kwa sababu aliahidiwa tabaka bora zaidi ya watu, hekima iliyo bora zaidi, kujua zaidi kuhusu jambo hilo kama angefanya jambo hili. "Wahudumu wetu wameelimika vizuri zaidi. Tuna tabaka bora zaidi."

Hakuna tabaka bora zaidi ya watu ulimwenguni kuliko wale wanaolishika Neno la Mungu. Hilo ndilo bora zaidi. Hilo ndilo tabaka pekee ambalo Mungu huangalia. Muda kidogo tu na labda Mungu atatu◌ruhusu tuingie ndani yake.

37 Ufalme Wake hauwezi kuahidi kitu ila mauti. Hilo tu ndilo alilo nalo. Yeye ndiye mwanzilishi wa mauti. Anaweza kuahidi uongo kwa sababu yeye ndiye baba wa uongo. Hawezi kukupa Uzima. Hawezi kukupa Mbingu, hana Mbingu ya kukupa.

Wazia jambo hilo! Neno moja, kutokumwamini Mungu kupitia ahadi ya ibilisi ama mitambo yake, Neno moja, linakupeleka kwenye mateso. Hivyo ndivyo ilivyoanza. Na kama Mungu, katika rehema Zake jinsi alivyo, angepeleka umati huu wa kuzimu duniani, na kusababisha watoto wadogo wenye njaa, kila namna ya mateso, na watu wanaokufa kwa njaa, na mauti duniani, kwa sababu Neno moja, hapo mwanzo, asingeweza kuliangalia tena na kukanyaga kutoka kwenye mateso haya yote? Je, asingeweza kufanya jambo hilo? Basi kama Yeye hakusamehe Neno moja pale, akijua ya kwamba haya yangekuwa matokeo yake, ni zaidi sana vipi asingalisamehe Neno moja pale wakati mtu binafsi atakapokuwa anayeteseka peke yake, yeye asiyeamini. Wazia jambo hilo, ni jambo kubwa mno.

38 Sasa, wakati Adamu na Hawa waliposikiliza uongo wa ibilisi, sanamu takatifu ya Mungu iliwaacha, ushirika wao na Mungu ulivunjwa. Ushirika wao wa umoja na Mungu ulivunjwa. Bakika ile ile waliposikiliza uongo wa ibilisi, hilo lilivunja ushirika wao. Na dakika ile ile mnaposikiliza uongo wa ibilisi, itavunja ushirika wenu. Hiyo ndiyo dakika ile ile unapoondoka Mbele za Mungu, kama alivyofanya, ni wakati uliposhindwa kuchukua Neno la Mungu jinsi lilivyo.

39 Sasa angalia, ninataka kuwauliza jambo fulani. Sote tunajua kuna Mungu. Na kama Mungu yuko sahihi sana na Neno Lake, na ameamua sana ya kwamba Yeye atawahukumu watu kwa Neno Lake, basi hana budi kuhifadhi Neno mahali fulani kuwahukumu nalo watu. Biblia hii ndiyo. Msisahau jambo hilo. Ni Biblia ambayo Mungu atawahukumu watu kwayo, kwa kuwa ilisema katika Ufunuo 22, "Yeye atakayeondoa Neno moja Kwake ama kuongeza neno moja Kwake."

Unaona, si kusema tu, "Vema, ni—ninaenda kanisani. Ninaamini. Ni—ni—ninamwamini Mungu." Mbona, kila ibilisi kuzimu anamwamini Yeye. Kila mmoja wao ni wa kidini, kila mmoja.

40 Lakini inachukua tu neno moja, ambalo linavunja ushirika papo hapo. Mnyororo hauna nguvu kuliko kiungo chake kilicho dhaifu sana. Kadiri udhaifu wako ulivyo juu ya kutokuamini Neno la Mungu, hapo ndipo unapotaka kuweka kiunganisho kipya, kilicho imara pamoja na hayo mengine. Kama unaamini Yesu Kristo anaokoa, basi huna budi kuweka kiungo hapo ndani ambacho huamini Yeye huponya. Kama unaamini alikuwa, lazima uamini Yeye ndiye. Haleluya! Kama unaamini Yeye alikuwa, na ukishangaa kama Yeye yuko, kiungo hicho kitavunjika, basi umepotea. Mnaona ninalomaanisha? Ni mkali, ni mgumu, bali ni Kweli. Huna budi kumwamini, kila Neno, kila kitu alichosema.

41 Sasa, unasema, "Vema, sasa, Ndugu Branham, vipi kuhusu madhehebu haya?" Vema, sasa sikilizeni. Kama wako pamoja na Neno hili, vema. Lakini kama wakilikana Neno hilo, basi si kweli, ni Ibilisi tena. Unaona?

"Vipi kuhusu hili kanisa hili fulani fulani?" Sijui kuhusu kanisa hilo. Jambo pekee nijualo ni Neno hili. Sasa, utaaminije kanisa wakati kuna madhehebu mia tisa na kitu tofauti, na kila moja likisema "dhehebu letu lina Kweli kabisa"?

Sasa ungeenda wapi? Huna budi kuwa na imani katika kitu fulani. Vema, unasema, "Nina imani katika Methodisti, katika Baptisti, katika Presbiteri, katika Lutheran, katika Pentekoste, katika Katoliki," chochote kile. Una imani katika madhehebu hayo, na, kama ni kinyume cha Neno, unafanya jambo lile lile alilofanya Hawa. Kweli kabisa! Unafanya jambo lile lile alilofanya, kuchukua Neno la Mungu na kulifanya …

42 "Vema, kuna tabaka bora zaidi ya watu wanaokwenda hapa. Ni jengo kubwa zaidi. Wao ni watu

werevu." Hilo halina uhusiano wowote nalo. Shetani ni mwerevu sana kuliko Hawa. Yeye hakuninii … hakuwa hata kwenye picha. Lakini yeye hakupaswa kuwa mwerevu, alipaswa kuwa mtiifu. Hatupaswi kuwa werevu. Yesu alisema watoto wa ulimwengu huu, ama, ufalme wa ulimwengu huu ni werevu sana, wana wa giza kuliko wana wa Nuru. Tunafananishwa na kondoo. Kondoo hata hawawezi kujiongoza wenyewe, hawana budi kuwa na mchungaji. Mungu hatutaki tuwe werevu, Yeye anataka tutegemee ufahamu Wake, amina, mahali tu anapoelekeza. Amina. Mnaona ile picha? Usizitegemee akili zako mwenyewe. Mithali 5, 3. Usizitegemee akili zako mwenyewe, tegemea ufahamu Wake. Haidhuru linaonekana ni kinyume jinsi gani, na jinsi taa zenye mwangaza zinavyoonekana kubwa hapa, msijali jambo hilo. Tegemea tu ufahamu Wake, yale aliyosema ni Kweli.

43 Sasa, umoja katika ushirika ulivunjwa kati ya Mungu na watoto Wake, dakika tu alipoacha kifungu kimoja kidogo, Neno moja dogo la Mungu. Kila mtu anayepata hilo, aseme "amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Si Biblia; useme, "Siamini Biblia hata kidogo. Ninaamini nusu Yake." Ilimbidi kuliamini lote, kila sehemu.

Si hilo tu, bali umoja kati ya mume na mke ulivunjwa. Siamini kuna ndoa yoyote inayoweza kuwa bila ya muungano kati ya mume na mke na Mungu. Hiyo ni kweli. Watawalea watoto ulimwenguni, na kuwafanya haramu, kuwapa sigara, wiski, kucheza karata machoni mwao, kunywa pombe mbele yao. Haidhuru wao ni waaminifu vipi kwa nadhiri zao za ndoa, hiyo ni kujuana kimwili, huo ni mwili. Lakini kuna roho mle ndani, hiyo roho ya baba mwenye dhambi na mama, haidhuru ni waaminifu jinsi gani kwa watoto wao, watakosea.

44 Vema, unasema, "Ninawajua wanaume na wanawake ambao hawakufundisha watoto wao jambo hilo, na hawakuwa Wakristo." Jambo lile lile la kutowaongoza kwa Kristo lilikuwa ni jambo baya sana waliloweza kufanya mbali na lingine; si kuwaongoza kwa Kristo, unaona. Kwa hiyo huwezi kuwa na muungano sahihi bila hilo. Ushirika ulivunjika.

Ndipo mara ushirika ulipovunjika kati ya Adamu na Hawa … Mara tu ushirika wao ulipovunjika kati ya Mungu na wao, ndipo ushirika wao kati yao ulivunjika.

Sikilizeni! Wakati wo wote kanisa linapovunja ushirika wake, kujitupa katika madhehebu, ushirika wa waaminio unavunjika. Hatuna budi kuamini kwa moyo mmoja, nia moja, na pamoja. Hivyo ndivyo walivyokuwa kabla muungano haujapata kamwe kufanywa kwenye Siku ya Pentekoste; moyo mmoja, nia moja, na pamoja. Na wakati unapolitupa kanisa katika madhehebu, utapata kila namna ya vipande - vipande ndani yake. Kwa sababu, baadhi ya hao watoto mle ndani watamwamini Mungu, watashikilia jambo lililo kweli, na hao wengine wataenda upande mwingine. Kwa hiyo, huna ushirika. Naam.

45 Nini? Mawazo yake yalibadilika. Loo, naam, mawazo yake yalibadilika. Ushirika wake na mumewe haukuwa sahihi. Walianza kupitisha pesa. Unaona? Mawazo yake kwa kweli yalibadilishwa. Kwa nini? Alikuwa na uhai wa ibilisi ndani yake. Kweli kabisa! Mara tu alipokosa kuliamini Neno la Mungu, alikubali maisha ya ibilisi kwa sababu alikubali mafundisho yake.

Ninaweza kuliimarisha hili papa hapa, lakini liko kwenye kanda. Nina hakika mnaelewa, Kanisa.

Yeye hakuliamini Neno la Mungu na likamtenga na Mungu, kwa sababu ndani yake papo hapo palikuwa na maisha ya Ibilisi. Alikuwa ameamini uongo wake, kasema, "Matunda ni mazuri," naye angeyala pamoja naye. Hiyo ni kweli.

46 Mimi sitashikilia Hili, nitaliacha lije hata hivyo. Siwezi kabisa. Hivi majuzi huko California, ninamaanisha kule Arizona, nilikuwa nikifundisha kanisani. Sijasema kamwe kitu chini ya uvuvio ambacho ilinibidi kukiondoa. Wahudumu wengi sana walinifuatilia kuhusu uzao wa Shetani, uzao wa nyoka. "Huyo mwanamke, alikuwa akila tofaa." A -ha! Hilo, vema, Kaini aliwazia jambo lile lile, aliingiza matunda ya shamba, unaona. Haikuwa tofaa! Alitambuaje alikuwa uchi? Tumekuwa tukipitia hilo. Kwa kweli lilikuwa ni jambo la kujuana kimwili. Hakika, ilikuwa, alitambua alikuwa uchi. Naye alipata mtoto kwa nyoka, ambaye hakuwa mtambaazi, alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote. Yeye alikuwa kitu cha pili kwa mwanadamu. Mwanadamu anaweza kupata nyani na sokwe—sokwe, na kadhalika, bali hawawezi kupata kiungo kinachowaunganisha mwanadamu na mnyama pamoja. Huyo hapo. Mungu alimlaani mpaka hawezi kurudi tena, hilo ni juu yake kwa ajili ya tendo hili baya alilofanya. Yeye alikuwa ni mbegu ya pekee ambayo ingechanganyikana.

47 Sasa, hivi majuzi, nikisimama, nikihubiri, kulikuwako na kundi la Wakatoliki katika wasikilizaji wangu, nami nikasema, "Ninyi Wakatoliki mnaomwita Yesu, ama, mnamwita Mariamu, hasa, 'mama wa Mungu,' Mungu anawezaje kuwa na mama wakati Yeye ni wa Milele? Hawezi kuwa na mama. Yesu hata hakuwa kitu cho chote kwa Mariamu, bali alikuwa tu … yeye alikuwa ni kiangulio kilichomtotoa."

Vema, sikuzote waliamini, nami nilikuwa na wazo lake mwenyewe miaka mingi iliyopita, ya kwamba ile —ile dhana ya usafi ilikuwa kwamba Mungu alimtia uvuli na kuweka seli ya damu mle ndani, bali yai lilitoka kwa mwanamke. Kama yai likitoka kwa mwanamke, hapana budi kutokee mhemko wa kuingiza yai kupitia

kwenye mrija hadi tumboni. Unaona unavyomfanyia Mungu? Unamfanya Yeye katika mchafuko wa kujuana kimwili. Mungu, aliyeumba seli ya damu, aliumba yai, pia. Daktari, hapana budi kuwe na chavua za kiume na za kike pia. Hiyo ni kweli.

48 Vema, basi, kama mwanamke huyu alitoa yai, basi Daudi angewezaje kusema "Sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu, wala sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu"? Basi kama yai la mwanamke lilikuwa katika Kristo, basi mtu huyo ana uhusiano wowote na sehemu Yake katika ufufuo, wakati imekamilika kabisa kwa Mungu. Kwa nini Mungu aliinua sehemu ya kujuana kimwili ya mtu? Katika ufufuo, kwa nini hakuuacha mwili Wake uone uharibifu? Kwa sababu alikuwa mtakatifu. Naye angewezaje kuwa mtakatifu kama angekuwa na mimba na Mariamu, na chavua ilikuwa imetoka kwa Mariamu, lile yai kupitia kwenye mrija kuingia tumboni? Ingebidi kuwe na msisimko fulani kulishusha yai. Ndipo mwanamke huyo angekuwa …

Vema, unasema, "Huenda yai hilo lilikuwa limekaa hapo. Ingewezekana." Lakini hiyo, kama ndivyo ilivyo, basi angalia kinachotendeka hapa, basi Yeye hakuwa Mungu moja kwa moja. Yeye hakuwa Mungu, kwa kuwa alikuwa mwanadamu. Lakini basi kama hiyo ni kweli, mwanamke huyo alikuwa na kitu fulani ndani yake. Na ile—ile mbegu halisi iliyotoka kwa Mariamu, ambayo ilitoka kwa mama yake, na mama yake, na mama yake, ilikuwa kitu cha kibinadamu kilichochanganywa ndani yake, kwa tamaa ya kibinadamu. Isingewezekana. La, bwana. Nikasema, "Yeye … yeye alikuwa tu …"

49 Kama tu vile unavyochukua tai na kumruhusu atage yai, na kuliweka chini ya kuku, kuku ataangua yai, yeye ni kiangulio tu. Lakini hakuna hata chembe moja juu yake, yule tai, huyo ni kuku. La, bwana. Yule kuku alikuwa … Ungeweza kumfunga kifaranga kidogo juu ya juu ya—ya yai la ndege, naye angeangua ndege, yule mtoto wa mbwa angeweza. Ni joto la mwili lililoangua yai.

Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Yesu. Mariamu alikuwa tu kiangulio. Mungu alimtumia kama anavyomtumia mwanamke mwingine yeyote. Alikuwa bikira, hakuwa amepata watoto. Yeye aliingia katika tumbo la uzazi la bikira, bali Mungu Muumba alilifanya yai na mbegu pia, akaliumba. Kwa hiyo, ilikuwa ni mimba safi.

50 Ninapotoka, bila shaka, mnajua ndugu wanaoningojea. Walisema, "Ndugu Branham, ninataka kukuuliza jambo fulani. Ulifanya kosa. Sasa tumekushika."

Nikasema, "Vema, hivyo ndivyo ninavyotaka, kushikwa."

Kisha akasema, "Ulifanya kosa kwa kusema jambo hili, ulipohubiri Uzao wa Nyoka. Sasa mnasema ya kwamba—yai hilo lilikuwa ni la … Mungu aliliumba, lile yai. Kilichotukia, tunaona hapa ya kwamba katika Mwanzo sura ya 3, Mungu alimwambia Mariamu, 'Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka.'"

Nikawaza, "Loo, jamani!" Sikuwahi kuhubiri jambo lolote maishani mwangu chini ya uvuvio ilinibidi kuliondoa, maana situmainii juu ya ufahamu wangu mwenyewe. Na kama ufahamu wangu ni kinyume cha Neno la Mungu, basi ufahamu wangu ni makosa. Haina budi kuwa ni Neno la Mungu. Kama sivyo, achana nalo, si kweli. Lakini sasa rarulia hilo chini ndilo jambo la kufanya. Moyoni mwangu, nilisema, "Baba wa Mbinguni, nisaidie. Sijui la kufanya hapa. Mtu huyo ana Maandiko, anaelekeza kidole chake, 'Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka.'"

51 Sasa, hili hapa! Roho Mtakatifu alisonga mbele. Ninaamini Yeye yule ambaye angeweza kumtia uvuli Mariamu, ambaye angeweza kuumba, Yeye pia anaweza kuweka Neno kinywani mwako. Ninamtegemea Yeye kila siku. Na daima ni Neno Lake. Yeye hawezi kusema ninii … kitu kilicho kinyume na Neno Lake. Halafu kama ukisema umetiwa mafuta, na kuhubiri dhidi ya Kweli za Mungu, basi si upako wa Roho Mtakatifu. Maana, wakati Roho Mtakatifu anapokutia uvuli, Yeye huleta kitu kile kile, maana ni Neno.

52 Sikilizeni. Ni kitu gani kilichotukia? Nikasema, "Vema, nataka kukuuliza jambo fulani. Mwanamke hana yai. Yeye hana mbegu. Alisema sasa, Yeye alisema si 'yai,' Yeye alisema 'uzao wako.' Naye hakuwa na mbegu."

Inahitaji muungano kufanya mbegu. Hiyo ni kweli, daktari? Haina budi kuwa. Kama una masazo mengi sana hapa, usingekuwa na uhai ndani yake, na kuyapanda hapa nje, ha—hayangeota kamwe, yangelala pale na kuoza. Wala usingeweza kupanda uhai bila kuwa na masazo. Kwa hiyo, unaona, kitu hicho chote ni muungano. Ninajaribu kuwaambia sasa kuhusu Kristo na Kanisa. Ni muungano. Unaona, kama mwanamke ni mbegu yake mwenyewe basi hahitaji ya kiume, yeye anaweza kumpata mtoto wake mwenyewe. Lakini yeye hawezi kuwa, hawezi kumpata mtoto huyo mpaka awe pamoja na wa kiume, kwa sababu inawachukua hao wawili kufanya uzao. Hiyo ni kweli? Panda mbegu isiyo na uhai ndani yake, uone kitakachotukia.

Kama vile walivyosema jambo hili mwanamke huyu akizaa mbwa hawa hapa. Unaona, isingekuwa hai. Isingewezekana, maana, unaona, chavua haitachanganyikana.

53 Sasa, angalia jambo hili sasa, yule—yule mwanamke hakuwa ni mbegu. Kwa hiyo, Yeye alisema, "Nitaweka uadui kati ya uzao wako na uzao wa nyoka." Akimwambia ya kwamba alikuwa akienda,

Mwenyewe, kumpa mbegu, si kwa kujuana kimwili, kingono. Alikuwa anaenda kuumba mbegu ndani yake. Vema, unasema, "Hiyo ingekuwa ni uzao Wake?" Naam. Ingekuwa ni ya Mariamu basi baada ya Yeye kumpa. Hili ndilo jicho langu, Yeye alinipa hili. Ni jicho langu, bali Yeye alinipa hilo. Huu ni mkono wangu, Yeye alinipa mimi. Hii ni sauti yangu, bali Yeye alinipa mimi. Unaona? Na uzao uliokuwako, Mariamu … haukuwa na uhusiano wo wote na Mariamu. Ilikuwa ni kitu ambacho Mungu alifanya Mwenyewe.

54 Kwa hiyo mbegu iliyokuwa ndani yake wakati huo, ilikuwa ni muungano wa tendo haramu, ambalo lilikuwa ni mauti. Alikuwa tayari amepewa mimba na uzao wa nyoka, maana alikuwa ameishi na … Naye akageuka na kusema, yeye mwenyewe, "Yule nyoka alinidanganya." Hiyo ni kweli. Na, mara, Kaini akaja.

Loo, tunajua alisema alipata mtoto kutoka kwa Mungu. Hakika, kila mtoto aliyezaliwa, haramu na cho chote kile, hana budi kuja kwa tendo la Mungu. Yeye Ndiye pekee anayeweza kuhuisha. Hakika. Hiyo ni kweli.

Unaona, alikuwa tayari kuwa mama. Na jambo hilo kamwe … ila tu kile lilichofanya, lilikuwa ni kuweka wazi jambo la uzao wa nyoka. "Mbegu iliyo ndani yako sasa imekusudiwa, tendo lako lisilo halali dhidi ya Neno Langu, pamoja na kitu hiki hapa, nawe sasa una uzao wa nyoka. Lakini nitakupa uzao kwa mimba iliyotakaswa, na Uzao Wake utakiponda kichwa cha nyoka, na kichwa chake kitaponda kisigino." Amina. Mwache tu Mungu awe nayo, kama ni Neno Lake atalitimiza.

55 Hiyo ndiyo sababu huna budi kuwa katika muungano na Mungu. Hiyo ndiyo sababu Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, baada ya Yesu kusema "wabatizeni katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," Petro aligeuka na kusema "wabatizeni katika Jina la Yesu Kristo," kwa sababu Jina ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni Bwana Yesu Kristo. Unaona jambo hilo? Inahitaji muungano.

Paulo hakuwa amemwona Petro, bali Roho Mtakatifu yeye yule, katika muungano ule ule (utukufu! , ilimfanya aseme jambo lile lile. "Je! Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Yeye alisema, "Hatujui kama kutakuwako."

Kasema, "Mlibatizwaje?"

Kasema, "Kwa Yohana."

Kasema, "Huna budi kubatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo." Nao wakampokea Roho Mtakatifu.

Ilikuwa ni kitu gani? Muungano, wakisema jambo lile lile Mungu asemalo! Na huko ndiko kuungama. Kukiri maana yake ni "kusema jambo lile lile." Naye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, kutenda yale aliyosema. Tunasema ni Kweli, Naye anatenda jambo Hilo. Loo, jamani! Haya basi. Hiyo hapo mimba.

56 Sasa angalia jinsi yeye—yeye—muungano wake kati yake na mumewe ulivunjwa. Unaona, upesi, mara tu Mungu aliposema "Adamu, ulifanyaje jambo hili?" Badala ya kulichukua kwa ajili ya mkewe, yeye alilirusha kwa mkewe. "Mwanamke uliyenipa." Muungano ukavunjika. Unaona?

Alifanya nini? Badala ya kumpenda mumewe na kusema Kweli, yeye alidanganya. Yeye—yeye—yeye—yeye alipaswa kusema, "Yeye hana hatia, nilimpa." Amina. Biblia ilisema, "Alimpa mumewe." Alipaswa kusema, "Mtu huyo hana hatia. Nilimpa kisha akala, lakini mimi ndiye niliyempa." Badala ya jambo hilo, yeye alimpa nyoka, njia ya karibu kabisa.

57 Hilo ndilo jambo lile lile wanalojaribu kufanya leo. Unaona, mume, mke, ndoa imevunjika. Mume na mke, ushirika ulivunjwa kati yao. Umoja wao ulivunjwa, umoja kati yao na Mungu ulivunjwa. Kitu hicho chote kilichafuliwa. Kwa nini? Kwa sababu Neno moja halikuaminiwa. Loo, ndugu, jamani! Naam, alipaswa kusema Kweli. Ule umoja pamoja naye na mumewe ulikuwa umekwisha, na umoja wao na Mungu alikuwa ameondoka. Na kila kanisa lisilochukua Neno lote la Mungu, jambo lile lile linatukia. Ninapenda hilo, sivyo?

58 Mwangalie mzaliwa wake wa kwanza, Kaini, muuaji, uongo, mdanganyifu, mwenye wivu, wivu kwa ndugu yake. Ndugu yake alishika Amri za Mungu, na Mungu alikuwa amefanya upatanisho kwa kuua sadaka na kuitoa kwa ajili yao. Angalia ujinga wa jambo hilo sasa, wa Shetani, aliyejaribu kubadilisha kitu fulani. Mungu, Biblia ilisema, alienda na kuwafanyia nguo za ngozi; kupata ngozi, kitu fulani kilikufa. Adamu alijaribu kujifanyia nguoi kwa majani ya mtini. Isingefaa, uhai wa mimea. Uhai, uhai unaosogea ulipaswa kufa. Kwa hiyo akaua hali ya chini ya uhai, na kusema mle ndani ya kwamba "Siku moja Maisha Yangu Mwenyewe yatatolewa kwa ajili yenu, Uhai halisi utakaopatikana katika muungano huu tena." Sasa, tutalifikia katika dakika chache, Mungu akipenda. "Unaona, haya hapa maisha ya mwana -kondoo. Sasa, jizungushie hii nawe na ufiche uchi wako." "Hupaswi kula matofaa"? Upuuzi! Unaona? "Jizungushie hii ngozi." Ilimbidi kuua kitu fulani.

59 Na mwana wa Shetani, hawakuja jinsi alivyotaka yeye, yeye alikuja. Hata hivyo unataka kusema jambo hilo, bali ilikuwa ni mwana wa Shetani, maana ule usafi wa Adamu kwa Mungu usingeweza kuleta kitu kama hicho. Angalia basi mwana wa Shetani, akijaribu kufanya upatanisho, akarudi na jambo lile lile ambalo watu wengi wanasema leo, lundo la matofaa na matunda ya nchi, kutoa upatanisho, dawa ya

kinga.

Na Habili mwenye haki alifanya nini? Alijua ya kwamba haikuwa kitu kama kula matofaa. Yeye alikuwa damu ya mama na baba yake, uhai wao. Kwa hiyo akamleta mwana -kondoo, kama tu vile Mungu alivyofanya. Haleluya! Yeye alitimiza Neno la Mungu, na Kaini alikuwa na wivu naye.

Jambo lile lile leo! Njoo katika hiyo sadaka ya damu, hilo Neno la Mungu jinsi hasa linavyosema, dumu moja kwa moja Nalo. Wengi wao wangeamini hiyo sadaka ya damu, hakika, lakini wakisema jambo lingine katika Neno, wao wanasema, "Loo, la, siamini hilo. A-ha, hiyo—hiyo ni kwa ajili ya siku nyingine." Pepo yule yule wa kale, hila ile ile ya kale! Ngojeni mpaka tutakapomaliza jambo hilo. Angalia, alishuka moja kwa moja vivyo hivyo.

60 Lakini Kaini, katika njia zake za kipumbavu, si mpumbavu sana, bali katika njia zake za udanganyifu, alidanganywa, na akaleta matunda. Adamu alitunza … Habili alilishika Neno la Mungu, akamleta mwana - kondoo. Mungu alisema, "Hiyo ni kweli, Adamu, umeweka … Ama, Habili, umelitimiza Neno Langu." "Kaini, ulijua haikuwa … Ni wapi nilichukua majani ya mtini kama baba yako alivyojaribu kufanya? Una lundo la tini ama zabibu ama matofaa ama chochote ulicho nacho hapa. Na sasa baba yako alichukua majani ya mti, kujaribu kufanya upatanisho, na hapa unajaribu kutoa tunda kutoka kwenye mti." Haikuwa hivyo! Ilikuwa ni damu kutoka kwa uhai.

61 Loo, Mungu aliishusha, kasema, "Hii hapa." Naye Habili alimtolea iliyo sahihi. Ndipo ndugu yake akamwonea wivu. Angalia kile alichofanya, alimwua ndugu yake. Mungu alimwinua mwingine; kama mauti, kuzikwa, na kufufuka kwa Kristo. Angalia. Mungu basi, ninii Yake … Yeye aliwaambia nini Adamu na Hawa? "Enendeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi." Tawanya wanadamu kote duniani, ili aweze kuwashughulikia mmoja mmoja mpaka aweze kuwarudisha pamoja. Kushughulika na watu, watu binafsi, kila mtu. Lakini hawakutaka iwe hivyo.

Usikose ufunuo huu. Mungu, hebu litendeke. Hebu ulione jinsi ninavyoliangalia.

62 Unaona, haikuwa hivyo, Mungu hashughuliki na mtu katika kundi. Mungu hashughuliki na wewe katika madhehebu. Yeye hushughulika nawe kama mtu binafsi, mtu binafsi. Kibinafsi tumebatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kwa pamoja tumebatizwa katika Mwili tunapobatizwa kwa Roho Mtakatifu. Kibinafsi, kila mmoja alibatizwa kwa Roho Mtakatifu, Mungu akishughulika na kila mmoja. Hilo lilikuwa ndilo kusudi Lake, kuwatawanya kote ulimwenguni apate kuwashughulika nao kibinafsi.

Lakini badala ya jambo hilo, ni jambo gani lililotukia? Ilimbidi Mungu kuwatenganisha watu wa Kaini na watu wa Sethi. Yeye alimfukuza Kaini. Aliwatenganisha ili aweze kulishughulikia kanisa Lake. Angalia. Kaini alitengwa. Sasa angalia. Mungu alimtenga Kaini mwovu wa Hawa na Sethi mtakatifu wa Adamu. Loo! Je! Yeye alifanya hivyo? Kupitia tendo lisilo halali, mwanamke huyu akiishi na mtu mwingine na akamzaa mtoto. Mungu alimtenga mtoto huyo na vizazi vyake na mtu huyu mwenye haki na mtakatifu, watoto wake.

Ni jambo lile lile leo, kutenganisha, waliotenganishwa, kuwapata, hawakuwa katika umoja. Wasingeweza kuwa na umoja. Je! Usiku unaweza kuwa na umoja na mchana? Je, mwamini anaweza kuwa na umoja na kafiri? Je! Mtu anayeamini Neno lote la Mungu anaweza kuwa na umoja pamoja nao ambao wanaamini tu sehemu ya Neno la Mungu? Mungu anataka watenganishaji.

63 Sasa, Kaini alikuwa mwana wa Hawa, alisema, "Nimepata mwana." Lakini Sethi alikuwa mwana wa Adamu. Naye Mungu akawatenganisha kwa sababu asingeweza … Mbona, wangeharibiana wao kwa wao, watoto waovu wa Kaini wangewapotosha watoto wazuri wa Sethi. Hiyo ni kweli.

Sasa angalia! Na ibilisi yule yule wa kale aliyemfanya Hawa kutokuamini Neno moja la Mungu, na kuwaambia wajitenge mmoja kwa mwingine na kuishi tofauti, kila mmoja, ibilisi yule yule aliingia miongoni mwao na kuwaleta pamoja tena. Mlilipata hilo? Sema "Amina" kama ulifanya hivyo. [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Aliwaleta pamoja tena chini ya muungano wa uongo, tendo la Mungu … dhidi ya mpango wa Mungu. Ni kitu gani kilichotukia? Alifanyaje jambo hilo? "Wana wa Mungu," Biblia ilisema, Mwanzo, "waliwaona binti za wanadamu." Wana wa Mungu, wana wa Sethi, waliwaona binti za wanadamu, watoto wa Kaini, jinsi walivyokuwa warembo. Hum! Na, walifanya nini, waliwaangukia! Nao wakaungana tena, kwa sababu ya urembo, kwamba "walikuwa wa kupendeza."

64 Jambo lile lile leo! Hili hapa, ndugu. Ninyi wanyonge wa Kipentekoste, ambao Mungu aliwatenganisha na kuwatuma mpate kuwa na madhehebu mengine! Hamwezi kuifanya pentekoste dhehebu. Aliwatuma mkawe watu Wake. Lakini mmeona makanisa makubwa mazuri na theolojia, mnazo wenyewe shule nyingi kubwa na kadhalika. Nanyi mlifanya nini? Mmewaunganisha watu wa Mungu tena na madhehebu, ambayo, msingi wake hasa ni Ukatoliki. Makanisa mazuri, makubwa, watu waliovalia vizuri, meya wa jiji na hao wengine wote wanakuja, wamevaa vizuri kuliko wote, wenye elimu bora kuliko wote, wanatheolojia wa hali ya juu, wanajua jinsi ya kufikia mahali ambapo kila mtu huvaa nguo za kupendeza sana, na mchungaji husimama kikamilifu kabisa mahali pake. Ni kitu gani? Mnaangalia mambo ambayo Mungu

aliyahukumu. Nanyi mmelichukua kanisa la Kipentekoste (Mungu, hebu na lipige kanda!) na mmeliunganisha katika madhehebu. Mungu kamwe hakutaka liunganishwe, Yeye alitaka litenganishwe; kamwe halijaungana na ulimwengu.

65 Ibilisi yule yule wa kale aliyemfanya Hawa kutokuamini Neno la Mungu na kufanya uovu wake, akarudi moja kwa moja na kuwachukua watoto wa Sethi na kuwaacha wawaone hawa wanawake warembo wa Kaini, nao wakaungana tena. Nao hawakuwa makafiri. Hawakuwa wakomunisti. La, la. Walikuwa waamini. Wakasema, "Sasa labda Bwana huenda akatenda jambo fulani." Ama, loo, hivi namna hiyo. Wao—wao walikuwa … Walifikiri walikuwa wakifanya yaliyo mema. Na Mungu ilimbidi kufanya nini? Futa kitu hicho chote, ilibidi akifute kitu hicho chote. Chini ya muungano wa uongo! Ilimbidi kutuma gharika na kuliangamiza kundi lote. Hukumu ikaja kwa ajili ya muungano huo wa uongo. Hukumu iliipiga Edeni kwa sababu ya muungano wa uongo.

Sasa, hivi nyoka alikuwa na uzao? Aibu kwako.

66 Muungano wa uongo ulileta hukumu duniani, kwa Hawa na Adamu, katika Edeni. Na muungano wa uongo ulileta gharika ya hukumu ya Mungu juu ya nchi kwa sababu binti za Kaini waliwachezea wana wa Mungu, nao wakaanguka kwa ajili ya hilo na kuungana pamoja tena. Haya basi. Muungano wa uongo, "Hakuna kitu kingeweza kutendeka." Mungu alifanya nini? Yeye aliharibu kitu hicho chote, yote isipokuwa mzee wa thamani Nuhu na familia yake. Yeye … waliungana pamoja.

Na tena baada ya jambo hilo, baada ya kifo cha Nuhu, na jamaa hiyo ya kiroho ya Nuhu, jambo la kwanza unajua, wana wa binadamu walianza kutazamana wao kwa wao tena. Walifanya nini? Walisema, "Sasa, sisi si makafiri, sote tunamwamini Mungu." Kwa hiyo wakampata jamaa, kwa kiongozi, askofu mkuu mashuhuri jina lake Nimrodi, nao wakajenga mnara. Hawakuwa makafiri. Waliamini kulikuwa na Mbingu. Waliamini kulikuwa na kuzimu. Waliamini katika hukumu. Lakini watoto wa Mungu pamoja na binti za wanadamu, tena, nao walijifanyia muungano, kwa uongo, na wakajenga kanisa kuu kubwa mno, dhehebu kubwa mno, na mahali pengine pote palipaswa ku—Babeli, ilikuwa ni kulipa kodi kwa hilo.

67 Nao wakasema, "Ninawaambia tunachoweza kufanya. Unajua sisi ni werevu." Walipata wapi hekima hiyo? Kutoka kwa Ibilisi. Hiyo ni kweli kabisa. Walilipata kutoka kwa ibilisi kama—kama vile Hawa alivyofanya. Umelipata kutoka kwa ibilisi. Kwa hiyo wakasema, "Tutajijengea dhehebu, tutampendeza Mungu. Nami nitawaambia yale tutakayofanya, tutakuwa na vipandio vya ngazi vidogo. Tutaruka na kuimba na kufurahi pamoja na malaika, na kurudi hapa chini na kuishi jinsi tunavyotaka." Ibilisi huyo angali anaishi. Unaona? Ilikuwa ni kinyume cha amri za Mungu. Hawakuzishika amri Zake. Mungu alifanya nini? Vema, walijenga mnara wa Babeli, wa uongo tena, kwa hiyo Mungu akawachanganya na kuwatenganisha.

68 Mungu alitengana tena na akamtuma Ibrahimu mzee mwema mwenyehaki, kasema, "Nitakuchukua tu na kukufanya taifa." Mungu aliwatenganisha. "Tokeni kati yao, Ibrahimu, acha kila kitu nyuma." Na Mungu kamwe hakumbariki mpaka walipoacha kila kitu nyuma, Lutu alikuwa wa mwisho. "Toka, Ibrahimu, jitenge na hao wasioamini. Nami nitawachukua na kuwafanya taifa. Nitawafanya watu watakaozishika amri Zangu. Nitawapa nafasi nyingine."

Mzee mwema Ibrahimu alienda kusafiri katika nchi ya kigeni. Hivyo ndivyo kila Ibrahimu anavyofanya, akikaa katika nchi ya kigeni. Nini? Kuamini ahadi ambayo haiwezekani, kunena kibinadamu. Unafikiri hao madaktari wa kisasa wa Kaini wangesema nini siku hiyo? "Whiu, jamani, mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, atapata mtoto kwa mkewe, tisini? Loo, ni jambo la dhihaka jinsi gani!" Lakini Ibrahimu aliamini Neno la Mungu. Na cho chote kilicho kinyume chake, aliita kana kwamba hakikuwako.

Ubatizo huu wote wa uongo, mihemuko ya uongo, upuuzi unaoendelea leo, wanasema haupo, amini Neno la Mungu na uendelee. Ni kikwazo tu kukuzuia usifikie kilicho halisi. Hiyo ni kweli. Songe mbele moja kwa moja, enyi watoto. Neno la Mungu, Mungu hutimiza Neno Lake. Sijali ni mambo mangapi bandia anayotupa Ibilisi huko nje, Mungu angali ana Neno la kweli Naye hulitimiza.

69 Ibrahimu aliita cho chote kinyume, kosa. Warumi, mlango wa 4, kama unaandika. Ibrahimu aliita kitu chochote kinyume cha Neno la Mungu, kana kwamba hakikuwako. Hiyo ni kweli. Yeye alimwamini Mungu, alikuwa na nguvu, haidhuru mwili wake ulidhoofika jinsi gani, jinsi ilionekana haiwezekani kwamba hautatendeka, Ibrahimu aliendelea kuliamini. Sasa, haikumlazimu kushuka kwenda madhabahuni na kusema, "Kama haliji sasa hivi, nitafanya … Sijui kama nitaamini au la." Ibrahimu alikaa nayo kwa muda wa miaka ishirini na mitano kabla haijaja, bali ilifika pale. Daima hufanya hivyo.

70 Ibrahimu, akaja Isaka; Isaka, akaja Yakobo; kutoka kwa Yakobo walitoka wale wazee wetu; kutoka kwa wale wazee wetu, wakaenda Misri; huko Misri, kulikua taifa. Ndipo wakati alipolikuza taifa Lake, mafanikio Yake, Yeye alifanya nini? Mungu aliwatenganisha tena. Kutokuamini na imani haziwezi kwenda pamoja. La, bwana. Yeye aliwatenganisha tena, kwa ajili ya walio Wake. Yeye aliwafanyia nini kuhakikisha kwamba waliongozwa vizuri? Sikilizeni kwa makini sasa, hatuna wakati mwingi zaidi sasa, labda dakika nyingine kumi na tano. Aliwaongoza karibu. Angalia, Yeye aliliinua taifa, akawaweka chini ya

waalimu na kadhalika. Walikuwa wakipigwa na kulia, na kulia na kuendelea. Lakini Mungu alikuwa akiangalia chini, alikumbuka kila ahadi aliyompa Ibrahimu. Siku moja Yeye—Yeye aliwazia … Yeye aliwafanyia nini? Alifanya nini alipowatenganisha? Yeye aliwapa sheria na akawapa nabii, akawapa Nguzo ya Moto. Yeye alifanya nini? (Ee Mungu!) Aliliweka kanisa Lake katika utaratibu. Nguzo ya Moto, Roho, kuwaongoza, nabii ambaye angewaambia Ukweli wa Neno Lake. Walikuwa tayari kwa safari wakati huo. Hilo si ni la ajabu?

71 Walitoka wakaenda jangwani, wakifanya ishara na maajabu, wakifungua Bahari ya Shamu, wakiita mapigo ya kuzimu kumwangukia Farao. Loo, jamani! Nguzo ya Moto ikitenda mbele zao, amina, iliwaongoza usiku na mchana. Haleluya! Nabii, mwaminifu kwa Neno hilo, akisimama pale akiwaweka kwenye mstari. Amina. Yeye alikuwa tayari kuwachukua watoto Wake wakati huo. Hiyo ilikuwa mara ya kwanza walipopata kuitwa kanisa. Ilikuwa ni mfano wa yale atakayofanya katika siku za mwisho. Tutalifikia hilo tena katika dakika moja. Yeye aliwaita watoke, akawapa sheria, akawapa Neno Lake, na akawapa nabii, akawapa ishara, na akawatuma nyikani. Aliwatenganisha na ulimwengu mwingine.

Walifanya nini? Waliona wanawake warembo wa Moabu, kanisa vuguvugu lenye miungu na miungu wa kike na kila kitu kingine. Walifanya nini? Wakaenda kwa ajili yao, wakaoa miongoni mwao. Hiyo ni kweli, kweli kabisa. Ninawazia hao wanawake wadogo wazuri Wamoabu walikuwa warembo kwelikweli.

72 Nina unabii ulioko nyumbani, moja ya siku hizi nitausoma. Nanyi mnashangaa kwa nini ninawafokea wanawake jinsi ninavyowafokea. Miaka thelathini iliyopita … Nina BWANA ASEMA HIVI! Miaka thelathini iliyopita wakati nilipoingia katika huduma, Yeye aliniambia ya kwamba aina ya wanawake ingekuja kwa uasherati sana na kuhesabiwa kuwa katika siku za mwisho wangekuwa kitu kilicho najisi sana duniani. Sawa! Alilianzisha hapo mwanzo na Shetani alimtumia mwishoni. Na angalia kile kinachotendeka, angalia miaka mingi iliyopita. Kasema, "Ataendelea kujivua nguo." Na akasema, "Kutakuwa tu na kundi dogo sana, la Wateule waliochaguliwa tangu zamani, watakaoponyoka hilo."

Wakati ono hilo lilipokuja, hilo liliniogopesha. Nikawaza, "Wanawake …" Nikarudi kwenye Biblia katika Isaya, naamini sura ya 5, nayo ikasema, "Tawi lililotoroka kutoka … binti za Sayuni, katika siku hiyo litakuwa zuri kwa Bwana."

73 Mwanamke fulani aliniandikia swali hivi majuzi, akasema, "Ndugu Branham!" Ama, la, ilikuwa ni mwanamume, mhudumu. Huenda akawa amesimama hapa asubuhi ya leo. Ametoka tu Ohio. Naye akasema, "Tunataka kusema jambo lile lile unalosema, lakini tumeona kitu fulani kwenye kanda zako ambacho si sahihi." Kwa hiyo Billy akaniletea hiyo barua. Kasema, "Kitu fulani kwenye kanda zenu," kasema, "kinapingana sana, Ndugu Branham, kwa Neno la Mungu. Nasi tunataka ku—tunataka kusema jambo lile lile." Kasema, "Swali moja nataka kuwaambia, hilo ni Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 11, na linasema hilo kuhusu kufunika kichwa kwa wanawake, na wanaume wasiwe na kifuniko." Kasema, "Tunaamini jambo hilo. Wanawake wanapaswa kuvaa kofia kanisani, na wanaume wanapaswa kuvua kofia zao kanisani." Kasema, "Tunaamini hayo ya kufunika kichwa, na kadhalika." Kisha akasema, "Basi swali lingine ni kwamba watu wanatujia na kusema Malaika wa Bwana anazungumza nawe kila kitu. Kila neno unalonena linatoka kwa Malaika wa Bwana. Na, Ndugu Branham, ni vigumu sana kupigana na kitu kama hicho," kasema,"kanisani mwangu." Kasema, "Tunataka kusema jambo lile lile. Sasa, Ndugu Branham, hivi huamini ya kwamba ulikosea kidogo pale?"

Nikaandika, "Ndugu yangu mpendwa, mimi sijakosea. Wakorintho wa Kwanza, sura ya 11, ilisema mwanamke anapaswa kufunika kichwa chake, na kwa nini. Ndipo kifungu cha 15 kikasema nywele zake ndefu amepewa kwa ajili ya kifuniko, si kofia." Hiyo roho ya Kikatoliki imelitawala kanisa kwa muda mrefu vya kutosha. Nywele zake ndefu ndicho kifuniko chake. Je! asili yenyewe . . .

74 Na angalia, ndipo swali likarudi, mtu fulani akaniuliza wakati fulani uliopita … Nitalielezea nikiwa katika hilo. Yeye alisema, "Vema, Biblia ilisema ya kwamba anapaswa kuwa na nywele ndefu kwa sababu ya malaika. Malaika wana uhusiano gani na mwanamke?"

Nikasema, "Malaika ni nini? Ni mjumbe." Paulo anasema nini? Kama mjumbe wa kweli, malaika kutoka kwa Mungu akipita, afadhali ungekuwa na nywele ndefu. Yeye atahukumu jambo hilo. Hiyo ni kweli. Ni wangapi wana … wanajua ya kwamba malaika ni mjumbe? Sawa kabisa. Mjumbe aliyetumwa kutoka kwa Mungu atahukumu hilo. Kasema, "Afadhali uwe na nywele ndefu, kwa sababu ya malaika." Hao wajumbe waliotumwa kutoka kwa Mungu wanakuja, watakihukumu kitu hicho. Naam, hakika, kwa sababu, mjumbe halisi kutoka kwa Mungu, malaika ameunganishwa na Mungu, na Neno Lake haliwezi kushindwa. Hiyo ni kweli kabisa. Mtakatifu Paulo alisema pale, ya kwamba kama hata Malaika kutoka Mbinguni akija kufundisha jambo lingine lo lote, na alaaniwe. Hiyo ni kweli. Sasa tunaona ya kwamba hiyo ni kweli, anapaswa kuwa na nywele ndefu, hicho ndicho kifuniko chake.

75 Lakini ninawazia wanawake hawa warembo wa Kimoabu walikuwa ni warembo sana, huenda walitengenezwa kama baadhi ya Mayezebeli wa kisasa wa siku hizi. Lakini, hata hivyo, si wanawake wote! Nafikiri mwanamke ambaye ni halisi ni kito. Mungu asifiwe kwa ajili ya mwanamke halisi. Ninyi ni wajakazi wa Mungu. Lakini mwanamke halisi ni kama mwanamume halisi, watalifuata Neno la Mungu

haidhuru ibilisi anasema nini, ama kitu chochote cha uongo.

Na kusema, "Mchungaji wetu alisema ni sawa kufanya jambo hili." Sijali kile mchungaji wako alisema. Kama ni kinyume na Neno la Mungu, hebu neno lake liwe uongo, na litimize Neno la Mungu. Jali ni dhehebu gani au yeye ni nani, kama ana cho chote cha kusema juu yake, mwambie alichunguze Neno la Mungu. Sawa kabisa.

76 Loo, jinsi ambavyo tungeweza kwenda huko chini na kumwona Mungu akiwatenganisha. Itatubidi kusimama kwa dakika moja tu. Nina baadhi ya Maandiko hapa ninayotaka kuyaacha, kuyafanya, kuharakisha kufikia mwisho. Ndipo wakati … ni jambo gani lililotukia wakati alipotukia kule, wakati wanawake Wamoabu? Ilimbidi Mungu kuwatenganisha tena. Yeye alifanya nini?

Ndipo akaja Yesu. Sasa ambapo tunakuja mahali fulani. Ndipo akaja Yesu, mfano wa Mungu uliodhihirishwa, uzao wa mwanamke, uliochukuliwa mimba na Mungu Mwenyewe. Mbunifu huyo mashuhuri alijiundia mwili. Haikumlazimu kukopa mbao kutoka kwa mtu yeyote, kutoka kwa mwanamke ama mwanamume. Alijijengea mwenyewe nyumba. Loo, jamani!

77 Ninafikiri juu ya Stefano siku ile aliposimama, kasema, "Enyi msiotahiriwa moyoni na masikioni, enyi wenye shingo ngumu. Daima mnampinga Roho Mtakatifu. Kama vile baba zenu walivyofanya, vivyo hivyo nanyi!" Kasema, "Sulemani alimjengea nyumba, bali Yeye Aliye juu haishi katika nyumba zilizojengwa kwa mikono, bali mwili ambao Wewe umeuandaa."

Haikubidi kukopa mbao zozote mahali popote. Waebrania, mlango wa 11, ninaamini katika kifungu cha 2 ama cha 3, inasema ya kwamba "Ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, vitu vilifanywa kwa vitu visivyoonekana." Mungu alisema tu, "Na iwe," na ikawa. Haikumlazimu kwenda kule na kusema, "Bw. Mwezi, ungeweza kunikopesha mbao kidogo? Bw.Nyota, ungeniacha nipate kalsiamu?" Mungu hafanyi hivyo.

78 Haikumlazimu kusema, "Mariamu, unanikopesha yai, ninataka kufanya mwili ili niweze kukaa ndani yake." Mungu Muumba alinena, naye alikuwa ni mama papo hapo. Hakuwa mama, alikuwa tu mwanamke akizaa Uzao Wake. Hiyo ni kweli. Kumbuka, yeye hakuwa mama yake Yesu. Ulimwengu ulisema hivyo. Nitafutie mahali pamoja katika Maandiko alipomwita mama yake. Sasa rudini kwenye Neno. "Mama wa Mungu," akuone aibu. Unaona?

Siku moja kulikuwa na watu fulani waliomwambia, wakasema, "Mama yako yuko nje anakutafuta."

Yeye alisema, "Mama Yangu ni nani?" Aliwatazama wanafunzi Wake, kasema, "Wao watendao mapenzi ya Baba Yangu ni mama Yangu."

Yeye hakuwa mama Yake, alikuwa kiangulio. Mungu angaliweza kutumia kitu kingine, bali alitaka kuchukua kilicho cha chini sana na kuonyesha kile angeweza kufanya nacho. Kukiinua juu, kufanya kitu kutoka kwenye hakuna, huyo ni Mungu.

Ile sura iliyodhihirishwa ikaja, Yesu, Yule asiye na hatia, Yule wa kupendeza, mzuri sana wa maelfu kumi, Nyinyoro ya Bonde, Ua la Uwandani, loo, Nyota ya Asubuhi. Yeye alikuwa nini? Alikuja kwa ajili gani? Sikilizeni kwa makini sasa. Kuanzisha tena umoja kati ya Mungu na mwanadamu. Loo, unaona jambo hilo, ndugu?

79 Minara yao yote ya Babeli na mambo yao mengine yote kule nyuma hayakufaa. Matunda yao yote ya bustani na kila kitu kilimchukiza Mungu. Kwa hiyo Mungu akashuka na akachukuliwa mimba katika tumbo la uzazi la mwanamke, kwa Yeye Mwenyewe, akajifanya mwili, na akawa Imanueli, Mungu pamoja nasi; si Myahudi wala Mmataifa, bali ni Mungu. Yeye hakuwa Myahudi, hakuwa Mmataifa, alikuwa Mungu. Na Mataifa walikuwa sawa Naye wakati wo wote, ila tu Yeye alijaribu kumtenganisha Myahudi kwa taifa. Yeye alijaribu kufanya kila kitu kuirudisha, na njia pekee ambayo angeweza kuthibitisha ilikuwa kumrudia mtu binafsi kama alivyokuwa hapo mwanzo. Hivyo ndivyo ilivyo leo, kwa mtu binafsi. Siyo kwa madhehebu, siyo kwa shirika, siyo kwa kundi la watu; bali kwa mtu binafsi. Angalia, kuanzisha tena umoja kati ya Mungu na mwanadamu.

80 Yeye alikuwa sadaka halisi ya dhambi. Kondoo, mbuzi, na kadhalika, wasingeweza kamwe kuondoa dhambi. Lakini uhai … Kwa sababu wakati dhabihu inapochinjwa na uhai wa mwana -kondoo, jambo lisilo na hatia sana, lisingeweza kurudi, uhai huo, juu ya mwamini, kwa sababu yeye alikuwa mwanadamu, mwenye nafsi, na kondoo hana nafsi.

Unaona, hakuna kitu kilicho na nafsi ila mwanadamu. Mungu aliweka … Yeye ni umbo la mnyama, hiyo ni kweli, bali Yeye aliweka nafsi juu yake. Hilo ndilo lililomfanya tofauti na wanyama. Alijua mema na mabaya wakati nafsi yake ilipomjia. Lakini yeye … Kumbuka wakati Mungu alipomuumba mtu katika mfano Wake Mwenyewe, na kisha akawa nafsi hai. Unaona, yeye akawa hivyo, akijua mema na mabaya.

81 Sasa angalia. Lakini sasa, katika jambo hili, Yesu alikuja na Yeye alikuwa Mungu. Si kwamba tu uhai

wa mtu mwingine unaweza kumrudia mtu mwingine, bali Uhai wenyewe wa Mungu, ukimfanya mwana wa Mungu, ukimrudisha katika muungano ule ule aliokuwa kabla ya kule kuanguka. Sasa tunapata umoja halisi.

Enyi watu, mtu fulani ananiambia, "Ndugu Branham, hivi wewe si wa umoja?" Siyo Umoja wa mashirika. Lakini mimi ni wa umoja na Kristo, mnaona, bali siyo wa Umoja wa shirika.

Alilipa deni ya dhambi. Sasa, kusudi apate umoja kati ya Mungu na mwanadamu, Yesu asingeweza kufanya hivyo mradi tu alikuwa hapa katika mwili wa nyama. Kwa hiyo ilimbidi awe dhabihu kamili ya dhambi kuondoa hatia ya mwamini, unaona, kuiondolea mbali ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kuingia ndani ya mwanadamu, na kumfanya mwanadamu na Mungu kuwa wa umoja tena. Unaona, ilibidi kuwe na kitu fulani cha kuanzisha tena.

82 Sasa, ni kitu gani kingeweza kuanzishwa tena? Wakati amri ya Mungu itakapotimizwa. Malaika angeweza kulitimiza? Hana damu. Mungu angeweza kulitimiza? Hakuwa na damu. Naye Mungu akafanyika mwili na damu kusudi apate kulipa deni vizuri na kuondoa dhambi, kwa sababu hiyo ndiyo njia pekee. Minara ya Babeli ikiwatenganisha kote duniani, kila kitu kingine, madhehebu na kadhalika yalikuwa yameshindwa kwa kila njia, yanachanganyikana pamoja, ulimwengu na kila kitu kingine, bali huu ulikuwa ni utengano wa jumla. Utukufu!

Sasa ninajisikia wa kidini. Vema, ninajisikia kama ninaweza kuchukua somo langu sasa na kuanza kuhubiri sasa hivi. Ninaanza tu kupata joto sasa ambapo ninaweza kuanza papa hapa, na ni wakati wangu wa kusimama. Mm! Labda nitaumaliza baadaye wakati mwingine, umoja wa Mungu na wanadamu. Mnaelewa? Wote wanaoelewa, semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

83 Unaona, hiyo ndiyo njia pekee ambayo mwanadamu angeweza kurudi katika hali yake ya asili tena, ni kwamba adhabu hiyo ya dhambi kulipwa. Adhabu ya dhambi ni nini? Mauti. "Mshahara wa dhambi ni mauti." Ndipo Mungu akasema, "Siku utakayokula, siku utakayofanya jambo hili, hiyo ndiyo siku utakayokufa." Na wakati ilipofanya hivyo, ilivunja uhusiano wake, ushirika na kila kitu kwa ajili ya mwanadamu, na isingeweza kurudi tena mpaka adhabu hiyo ilipolipwa. Na hakuna mtu aliyestahili kulipia, kwa sababu kila mtu alianguka pamoja na mwanadamu, maana kila kiumbe kiko chini ya mwanadamu, naye alikuwa ameanguka. Utukufu! Loo, ndugu!

84 Ndugu Mac, sikuona ukiketi pale, Mungu akubariki. Tunaamini jambo hili, Ndugu Mac. "Ingia chini ya hukumu ya mauti." Ndugu Mac hapa alikuwa mchungaji hapa maskanini wakati nilipoondoka. Naam. Sasa, maskini Mbatisti mwingine mzuri, Mbaptisti wa Kimishenari kule chini aliye na Roho Mtakatifu. Unaona? Angalia sasa, waliingia katika umoja na Mungu.

85 Sasa, tunapoona jambo hili, tunaona adhabu haina budi kulipwa, na hakuna … Hali ya juu sana ya uhai wa mnyama ni mwanadamu, na mwanadamu alianguka, mwenyewe. Kwa hiyo mtu mmoja anawezaje kumwokoa mwingine? Ilimchukua Mungu. Naye Mungu, katika Roho, asingeweza kufa. Kwa hiyo, "ilimbidi Mungu kujishusha chini kidogo kuliko Malaika," Waebrania sura ya 1, kifungu cha kwanza. Ilibidi ajifanye duni kuliko Malaika kusudi apate mauti, kulipa adhabu, kuleta umoja kati ya mwanadamu na Mungu tena, ili Roho Mtakatifu aweze kurudi.

Deni la dhambi lililipwa. Ilimbidi Yesu kufanya jambo hili kumrudisha yule—yule—Roho Mtakatifu, kuwaunganisha watu tena kama ilivyokuwa katika Bustani ya Edeni. Deni ililipwa wakati Yesu alipokufa. Hilo lilitosha. Amina, ndugu! Kama ningaliweza tu kulipata lizame ndani, mnaona. Deni limelipwa. Haleluya kwa Mwana -Kondoo! Deni limelipwa. Na kila mwanamume na mwanamke anayenisikia asubuhi hii, ama atanisikia kwa kanda, adhabu yako imelipwa. Msiache kuliamini Neno la Mungu tena. Rudini kwenye Neno! Msiamini … Yeye alikuwa Neno. Utukufu! Ninajisikia kama kupaza sauti, ni kweli. Adhabu imelipwa. Yote yamekwisha. Si ajabu Malaika walipiga makelele na kuimba, nyimbo za Mbinguni zinasikika. Naam, bwana, kondoo aliyepotea alipatikana! Upatanisho ulifanywa kwa ajili yake apate kurejeshwa tena, maji ya utenganisho, Neno la Mungu linalomwosha kutokana na uovu wake, wakati Neno lilipokufa mahali pangu na kufufuka tena na kuwa mkuu maishani mwangu, moyoni mwangu. Amina. Adhabu imelipwa! Imekwisha. Tumekombolewa.

86 Si kwa kanisa Katoliki; ingawa sisi ni katoliki sahihi, katoliki ya kimitume. Naam, bwana. Siyo Katoliki ya Kirumi pamoja na mafundisho yao ya sharti, wanalikana Neno hili kwa mafundisho yao ya sharti; kila kitu ni fundisho lako la sharti, si Neno. Mmethodisti, Mbaptisti, aibu kwenu, wapendao uovu kuliko kumpenda Mungu. Wapendao anasa, wanaotafuta ulimwengu, anasa, nguruwe waliochinjwa kwa ajili ya zizi. Ibilisi anatuma vyombo vyake huko nje akivisokomeza vitu hivyo ndani yako kama Shetani alivyofanya katika Bustani ya Edeni. "Vema, wahudumu wetu wote wana elimu. Wao wana Ph.D., LL.D." Hilo halimaanishi kitu. Kataa Neno hilo, ingali ni ujanja wa ibilisi. Nimewathibitishieni kwa Neno asubuhi ya leo, iwe juu yenu tangu sasa na kuendelea.

87 Wanafunzi, hata wakitembea pamoja na Yesu, hawakuwa na umoja. Hawakuwa na umoja wowote. La, wao walisema, "Ni nani atakayekuwa askofu baada ya jambo hili. Ni nani aliye mkuu kati yetu?" Hata

wasingeweza kumwamini Yesu. Hawakuweza kumfahamu. "Wewe wanena kwa mafumbo. Tuambie dhahiri unachomaanisha." Hakukuwa na umoja kati ya Yesu na wanafunzi, au wanafunzi kwa Yesu, na wanafunzi mmoja kwa mwingine.

Haidhuru, hilo linakuonyesha, ndugu. Sikilizeni kwa makini sasa, ninataka jambo hili liingie ndani kabisa ya moyo wako. Unaona? Mungu ana mpango. Nje ya mpango huo, sijali ni hekima kiasi gani iliyo nyuma yake, ni kiasi gani cha mamilioni ya dola za majengo, ni shule ngapi za theolojia, ni watu wangapi watakatifu na watakatifu hawa, na watakatifu, watakatifu, watakatifu, haileti tofauti yoyote. wote, kama Neno moja la Biblia ya Mungu limekataliwa, ni la Ibilisi. Sasa, nimewathibitishia jambo hilo kwa Neno lililoandikwa la Mungu, kutoka Agano Jipya hadi la Kale, nami nitamleta hadi siku kama mkiketi tu pamoja nami kwa dakika chache.

88 Wanafunzi waliotembea bega kwa bega pamoja na Yesu, walilala pamoja Naye, walikula pamoja Naye, waliangalia miujiza Yake, na kushirikiana Naye, karibu sana kama ndugu ye yote alivyoweza kuwa, na hata hivyo hawakuwa nao. Hawakustahili kuhubiri Injili. Yesu alisema, "Msihubiri tena, hata msijaribu. Ninyi ngojeni kule kwenye mji wa Yerusalemu. Nitawatumia ahadi, mliopewa, juu yenu. Hilo litakuunganisha wakati huo."

"Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba watakuwa mmoja kama tu Wewe na Mimi tulivyo Mmoja. Nami …" "Kama vile Baba Yangu alivyonituma niihubiri Injili, vivyo hivyo na Mimi nawatuma ninyi."

Na Baba yule yule aliyemtuma Mwana, alikuja katika Mwana. Umoja ni mmoja. Yeye alisema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama kazi Zangu ninazofanya zinanena kwa sauti kubwa sana, ninyi ni viziwi kabisa, bubu na vipofu kama hamzioni." Loo, ndugu, whiu! Kasema, "Enyi wanafiki! Unaweza kutambua uso wa mbingu, lakini ishara za wakati huu huwezi kuzitambua. Kama mngalinijua Mimi, mngaliijua siku Yangu. Vyema Isaya alinena habari zako. Una masikio, na wewe ni kiziwi sana huwezi kusikia. Macho, na vipofu sana huwezi kuona!"

Vyema Mtume Paulo alisema, "Katika siku za mwisho watakuwa na mfano wa utauwa na kukana Nguvu zake," na Maandiko baada ya Maandiko, yale yatakayotendeka katika madhehebu haya katika siku za mwisho. Ndipo wanashangaa ni kwa nini ninapaza sauti dhidi ya mfumo huo wa ulitengenezwa na mwanadamu wa ibilisi. Unawaona hao watoto wa thamani wakishawishiwa huko nje kama kondoo wakienda machinjioni. Walete nje, Bwana!

89 Naam, wanafunzi hawakuwa na umoja. Hawakuweza kumwelewa Yesu. Wakasema, "Aa, ni nani awezaye kufahamu mambo haya?" Unaona, Mungu hakuwa ndani yao bado. Walikuwa tu wamehusishwa katika ushirika. Wao walijiuhusisha tu Naye. Hao ni watu wengi wazuri leo. Hawakunywa, kusema uongo, kuiba, chochote, bali hawakuwa na huo umoja wa Mungu. Hawakuwa wamoja na Mungu bado. Unaona, wasingeweza. Loo, walifanya miujiza. Waliwatoa pepo. Hilo si—hilo si …

Nilisoma makala fulani kwenye gazeti hivi majuzi kuhusu hilo, kuhusu kutoa pepo. Watu wanasema, "Loo, ndugu, ninakwambia, hivyo ndivyo ilivyo." Hilo silo! Mtu anayemfukuza pepo na kukana Neno la Mungu, ni mwongo. Naam, bwana. Yeye anasema anatoa pepo. Wanadai wanafanya hivyo. Hawezi kufanya hivyo ikiwa hayuko pamoja na Neno la Mungu. Yesu alisema hivyo.

90 Sasa, ndipo Pentekoste ikaja, Mungu akawafanya mmoja tena. Loo, jamani! Ndipo wakawa na umoja na Mungu. Mungu alikuwa ndani yao. Sasa, Matendo, kama unayaandika, Matendo 4:32, Biblia ilisema ya kwamba "Walikuwa na moyo mmoja, nafsi moja, na nia moja." Loo, ndugu. Kwa nini? Walikuwa wamerejeshwa kwenye asili tena. Kitu pekee walichokuwa wameachwa kuachilia kilikuwa ni mji wa kale, ama waliishi hapa, mwili wa kale ulioitwa mji ama hekalu, ambao waliishi humu, ambao ulibidi uoze, kwa sababu hauna budi kufa na kuharibika. . Lakini katika roho na uhai, na katika kusudi na katika ono, na kila kitu, walikuwa mmoja na Mungu.

Loo, Adamu, rafiki yangu aliyefadhaika, usimwache Shetani akwambie uongo wake tena. Usiache jambo hilo litukie. Usimwache Shetani akwambie ya kwamba Neno halimaanishi tu kile linachosema. Hiyo ni kweli. Neno linamaanisha … Naam, hapa si …

91 Nilikuwa nikizungumza juu ya ubatizo wa Jina la Yesu Kristo. Hiyo ni kweli, ufunuo wa hilo umekuja. Hiyo ni Kweli. Lakini kundi la watu lilifanya nini? Walilikusanya papa hapa na kuweka madhehebu kutoka kwake, wakafanya mnara mwingine wa Babeli. Jambo lile lile, liliitupa moja kwa moja ndani yake. Hakika. Luther alifanya jambo lile lile. Wesley alifanya jambo lile lile, John Smith alifanya jambo lile lile, Alexander Campbell alifanya jambo lile lile. Pentekoste ilifanya jambo lile lile. Mungu hushughulika na watu binafsi wanaotunza Neno Lake. Mpango pekee wa Mungu wa kuwaleta waamini Kwake, katika umoja wa kweli, ni kumpokea Roho Mtakatifu. Basi hivi ndivyo …

Unasema, "Vema, Ndugu Branham, nilinena kwa lugha. Nikapaza sauti. Nilifanya jambo hili." Kama ungali una roho ya namna hiyo na kulikana Neno la Mungu, huna Neno la Mungu ndani yako, huna Roho. Kama utaketi na kusikia Kweli ikihubiriwa, na kuiangalia katika Biblia na kuona kwamba ni Kweli, halafu

unakataa kufanya jambo hilo, huyo si Roho wa Mungu. Sijali ulinena kwa lugha kiasi gani, ulipiga makelele kiasi gani, ulikuwa mfuasi wa makanisa mangapi, ama ulibatizwa mara ngapi, ama cho chote kile. Neno ni Kweli. Hilo ndilo linalothibitisha kweli. Kama una kweli hizi zingine zote halafu ukiwa na Neno, amina, basi unajua unarudi nyumbani.

92 Mungu yule aliyeandika Biblia anawezaje kugeuka na kuweka kibadala kwa ajili ya Neno Lake? Ninyi Wakatoliki mliosema ya kwamba Petro alizikwa kanisani mwenu, na roho yake inawapa haki za kuondoa dhambi na kadhalika, Petro angewezaje, Myahudi, kustahimili kuwa na sanamu kanisani? Petro angewezaje kukataa kusema ya kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu umekuja, naye alinena kwa lugha, na mambo hayo yote yenye nguvu aliyofanya, na kugeuka na kusema chukua mkate mwembamba kidogo, na Mungu yuko katika mkate huo mwembamba? Loo, ni ujinga, ujinga wa kiroho!

Vema, sasa, ninyi Waprotestanti vivyo hivyo, mnatembea na kupeana mikono na mhubiri, na kusema, "Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi," na kurudi nyuma na kuishi maisha ya aina yoyote kutoka kwake, na kuendelea moja kwa moja. kuishi pamoja na ulimwengu. Mnara mwingine wa Babeli.

93 Tunafikia mwisho sasa. Tazama. Mungu alimtuma Roho Mtakatifu, na Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe. Yeye Ndiye atakayefanya umoja kati ya Mungu na mwanadamu. Hebu na tuone. Sasa hebu na tufanye hivyo. Sasa nataka usikivu wenu usiogawanyiko kwa dakika tano zijazo au zaidi. Tazama.

Mwanadamu chini ya mpango wa Ibilisi amejaribu kulifanya kanisa kuwa katika umoja. Wamejaribu sasa kulielimisha kanisa katika umoja, mnajua hilo, kupitia elimu, kupitia dhehebu. Wanajaribu sasa hivi, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, wanajaribu kuwaleta Wakatoliki wote na Waprotestanti pamoja na kuwafanya mmoja. Ni kitu gani? Mpango wa ibilisi!

Unasema, "Wewe ni mdogo sana kusema hivyo." Mimi ni mdogo sana, bali Neno la Mungu wangu ni kubwa mno, nitawaambia jambo hilo. Mbingu na nchi zitapita, bali halitapita. Si yeye anayesema jambo hilo, ni Yeye yule—Yeye ambaye—Yeye aliyesema kwanza. Ninasema tu yale aliyosema, ninakiri Neno Lake.

Ni chini ya Ibilisi! Imethibitishwa katika Neno hapa, moja kwa moja asubuhi hii mbele yenu, ya kwamba ni ya ibilisi. Lolote la madhehebu hayo ni. Mwanadamu, chini ya mpango wa Ibilisi, akijaribu kuwafanya watu wawe madhehebu kwa umoja.

94 "Ninyi nyote mje kujiunga na Assemblies of God. Jiunge na Umoja. Jiunge na Kanisa la Mungu. Jiunge na Methodisti. Sisi sote ni mmoja." Ninyi kundi la wanafiki, mkiwa na mfano wa utauwa na mnakana Nguvu zake. Nalo Neno la Mungu likatetemesha moja kwa moja mbele zenu, nanyi mnaogopa kulishambulia. Kwa nini Mungu asijionyeshe Mwenyewe basi, kama uko pamoja na Mungu? Kwa nini usifanye kazi za Mungu? Unawezaje kuwa na umbo hilo, na kuzunguka na kumkana, hata ukiziita kazi halisi za Mungu Beelzebuli? Inaonyesha, ninyi kundi la washiriki wa kanisa walioelimika! Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi!" Sawa! Nina hakika mnafahamu ninalomaanisha. Hakika. Kwa nini mtu fulani asilishambulie? Unajua Mungu yuko nyuma Yake. Mungu atatenda kazi na Neno Lake.

95 Mwanadamu akifanya hivyo, inajenga mnara mwingine wa Babeli. Yeye anafanya nini? Wanajaribu kuonyesha … Angalia katika Baraza hili la Makanisa Ulimwenguni sasa. Waanglikana, Katoliki ya Kirumi, Wamethodisti, Wapresbiteri, Wapentekoste, na wote wameungana pamoja, Sayansi ya Kikristo, na madhehebu mengi ambayo hata yanakana kuzaliwa na bikira, yanayokana Uungu wa Yesu, yanamfanya Yeye watu watatu, yakijaribu kuabudu miungu watatu, kukataa kuzaliwa na bikira. Wengine wao wanaikana hiyo Damu. Baadhi yao wanakana miujiza Yake. Wote wanakana, karibia. Halafu basi—halafu jaribu kuunganisha kitu kama hicho pamoja, unawezaje kufanya hivyo? Ni mnara wa wakibinadamu. Utaanguka kama Babeli ilivyoanguka.

96 Lakini Mungu alisema, "Si kwa nguvu, si kwa uweza; kwa Roho Wangu, asema Bwana. Hivyo ndivyo nitakavyoliunganisha Kanisa Langu. Si kwa madhehebu, si kwa elimu, si kwa wanatheolojia; bali kwa Roho Wangu, asema Bwana, nitawakusanya kondoo Wangu pamoja." Loo, jamani! Na wakati anapofanya hivyo, ni jambo gani linalotukia? Na ishara Zake zitashuhudia vivyo hivyo. Hivyo ndivyo Israeli walivyoweza kusema, kabla hawajachanganyikana na Moabu. Kulikuwa na Nguzo ya Moto juu yao. Naam, bwana. Atafanya nini? Yeye atashuhudia, ushuhuda wa aina ile ile. Lakini baada ya wao kujitenga na kadhalika na Mungu, kutenganisha umoja wao kati yao na Mungu, na kuingia pamoja na Moabu na hao wengine, ushindi wote ulishindwa. Walikaa nyikani kwa miaka arobaini zaidi, mpaka Mungu akainua kundi lingine kwenda kule na kukamilisha mpango Wake. Hivyo ndivyo walivyofanya hasa.

97 Sasa angalia. Lakini wakati Mungu anapolileta kanisa pamoja na Roho Wake, watakuwa na ishara Zake za Mungu aliye hai miongoni mwao. Ni ishara za namna gani? Wakati Mungu alipotenganisha Israeli toka Misri, Mungu aliwapa Musa na Israeli ishara ya Nguzo ya Moto. Hiyo ni kweli? Nabii. Wakati alipomtenga Ibrahimu na Lutu, kulikuwako na Malaika aliyemjia, ambaye angeweza kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Ishara! Haleluya.

Sasa madhehebu haya yaliyoshikwa katika kanisa hili, yakijaribu kufanya umoja kama vile kule Misri, kama huko chini—katika Edeni, na kadhalika, chini ya ushawishi huu mkuu walioko.

Lakini, angalieni, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Wakati Mungu alipowatenganisha Israeli, Yeye aliwapa ishara ya Kimbinguni, Nguzo ya Moto. Yeye aliwapa nabii. Yeye alimfanyia nini Ibrahimu? Yeye hufanya nini kila wakati? Nionyeshe nabii aliyechaguliwa na Mungu miongoni mwao. Yeye aliweka kanisa Lake pamoja na mitume na manabii na waalimu na wainjilisti. Haleluya! Haya basi. Kanisa, tena, kama Yeye alivyowaita Israeli watoke. Niliwaambia ningelirudia. Naam, bwana.

Hakuna manabii walioteuliwa na Mungu miongoni mwao, la, bwana, kama walivyokuwa pamoja na Israeli na hao wengine. Ni kitu gani? Mnara wa ibilisi tena.

98 Sasa, kule Kuja kumekaribia sana, kule Kuja kwa Pili kwa Yesu, Yeye anawakusanya Wateule Wake pamoja. Ninaamini jambo hilo. Loo, watatoka Mashariki na Magharibi. Palipo na mzoga, tai watakusanyika. Loo, jamani, ni kitu gani? Yeye ana umoja Wake, umoja Wake wa kweli, akijionyesha Mwenyewe miongoni mwao; kutoka katika kila madhehebu, akiwaleta Wateule Wake pamoja kutoka kila namna ya makanisa, kutoka kila mahali, akiwaleta watoto Wake, akipatana moja kwa moja na Neno Lake. Nini?

Sasa, kule Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia sana, kule kuja kwa hukumu, Yeye anawaita Wateule Wake pamoja katika umoja na Yeye Mwenyewe, pamoja na huduma ile ile aliyokuwa nayo. Mnajua jinsi nilivyoumba katika Nyakati za Kanisa, hapa si muda mrefu uliopita, kuhusu—ule mnara mkubwa uliojengwa, ulioitwa piramidi, bali jiwe la kichwa halikuwekwa juu yake. Kumbukeni jinsi Walutheri walivyokuja, halafu Wawesley katika uchache, halafu hata Pentekoste. Na sasa kile anachofanya, akitoa wito huo. Yeye alifanya nini? Yeye aliwaita Wateule, kuwafanya Waluteri; Yeye aliwaita Wateule, kutoka kwa Walutheri, kuwafanya Wawesley; Yeye aliwaita Wateule, kutoka katika hayo, kuwafanya Wapentekoste; sasa Yeye anawaita Wapentekoste Wateule watoke, kulifanya jiwe la kichwa liingie ndani yake. Huduma ya namna ile ile ikiangukia moja kwa moja, kuwaita watoto Wake kutoka madhehebu yote na kila tabaka la watu.

99 Yeye amefanya nini? Yeye ameweka pamoja nao waalimu wa kweli, manabii wa kweli wanaodumu na Neno Lake, Biblia. "Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu," alisema Yesu. Kama hiyo ilikuwa Sauti Yake wakati huo, ni Sauti Yake sasa. Cho chote kilicho kinyume na Sauti hiyo, si chakula cha kondoo. Hawataifuata. Loo, ndugu. Kutoka Mashariki, kutoka Magharibi, kutoka katika kila dhehebu, kutoka katika kila dhehebu, wametoka Mashariki na Magharibi, wakikusanyika pamoja! "Tutakula pamoja na Mfalme, kula kama wageni Wake, jinsi wasafiri hawa walivyobarikiwa! Kuutazama uso Wake uliotukuka ukimeka kwa upendo wa Kiungu; washiriki wenye neema Yake, kama vito katika taji Yake kung'aa. Yesu yuaja hivi karibuni, majaribu yetu yatakwisha." Haleluya! "Vipi kama Bwana wetu wakati huu angekuja kwa ajili ya wale walio huru na dhambi? Basi ingekuletea furaha, ama huzuni na kukata tamaa kukuu? Lakini Bwana wetu atakapokuja katika utukufu, tutakutana Naye juu hewani." Haleluya! Naam, bwana.

100 Ni kitu gani? Pamoja na waalimu waliotumwa na Mungu ambao watadumu moja kwa moja na Neno, kwa Kanisa halisi, wasisogee hata dakika moja haidhuru madhehebu yasemaje. Hawajaunganishwa nayo. Manabii; siyo imani ya kujifanya, wanaojiita, bali nabii halisi ana BWANA ASEMA HIVI, na moja kwa moja kwenye nukta kila wakati. Hivyo ndivyo alivyotuma katika Kanisa Lake. Hivyo ndivyo alivyosema angefanya. Anaamini Neno; si kanuni za imani, si fundisho la sharti, bali Neno. Na, kwa kufanya jambo hili, Yeye hujionyesha Mwenyewe ndani yao kwa kuthibitisha Neno Lake, akifanya Uhai ule ule alioishi mara moja, kuishi tena, akilitimiza Neno Lake. Loo, jamani!

101 Sikilizeni kwa makini. I Wakorintho wa Kwanza 4:20, inasema, "Ufalme wa Mungu ni Neno Lake lililofanywa nguvu." Ukitaka kuandika hayo, I Wakorintho 4:20. Ufalme wa Mungu ni Neno la Mungu lililofanywa nguvu. Ufalme wa Mungu ni nini? Uko ndani yako. Ufalme umo ndani yako. Na wakati Neno linapoingia mle ndani, Neno hili linaanzisha nini? Linajigeuza lenyewe kuwa nguvu, na kulifanya Hilo liseme vile hasa Lilivyosema.

Huwezi kusema "Linasema hivi," na linasema Hili, na kulifanya litende kazi. Huna budi kusema jambo lile lile linalosema. Hilo linafanya maungamo. Sio kusema, "Vema, limeng'arishwa vizuri kidogo hapa, nitakuwa na hekima zaidi, nitakuwa na kusimama bora zaidi hapa."

Wewe dumu na Neno. Hilo hapo, unaona. Na inalifanya Hilo nguvu. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, "Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu ndani yenu." La, samahani, hilo silo alilosema pale. Yeye alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Kama mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo nanyi mtatendewa. Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu."

102 Ni kitu gani? Huna budi kuambatana na Neno, ujiondoe mwenyewe. Nina shawishika ya kwamba wengi wetu, marafiki, tumempokea Roho Mtakatifu, bali tumepokea tu Roho Mtakatifu wa kutosha ndani yetu kutufanya mahali ambapo hatutaki kusema uongo, hatutaki kuiba, sitaki kufanya chochote. Lakini Mungu anataka kujaza kila uzi wa Kanisa Lake, Yeye anataka kujaza mawazo yako na Yeye anataka

kujaza akili yako. Yeye anataka kukujaza kila sehemu yako, kukufanya tu kabisa, uwe mfu kabisa kwako mwenyewe au kwa mawazo yako, uliejitolea tu katika Mungu hata Neno Lake linaishi moja kwa moja kupitia kwako. Hujui kitu kingine ila Neno la Mungu, dumu tu na Neno Lake, ni Uzima. "Maneno Yangu ni Uzima," alisema Yesu. Yeye amewekwa pamoja nao, waalimu wakiamini Biblia, manabii wanaosema Kweli, wanaosema, wanaonyesha unabii ule ule ambao daima wameuonesha kote katika nyakati. Yeye amefanya nini? Yeye anajionyesha hai miongoni mwao, akithibitisha Neno Lake. Neno Lake, Ufalme wa Mungu ni Neno la Mungu lililofanywa nguvu.

103 Wakati, madhehebu haya yanategemea mawazo ya kibinadamu, juu ya hoja za kibinadamu. Sikilizeni kwa makini sasa. Wao … Hatupaswi kutegemea hoja za kibinadamu. Mithali, sura ya 3, aya ya 5, ilisema, "Usizitegemee akili zako mwenyewe." Unaona? Usifanye hivyo, haidhuru Neno la Mungu linaonekanaje.

Unasema, "Vema, yaonekana kana kwamba ni nzuri namna hii."

Hivyo sivyo ilivyo. Ni Neno la Mungu, lichukue jinsi alivyolisema. Hawa alisema … Shetani alimwambia Hawa, "Ninajua Mungu alisema Hilo, lakini kwa kweli halimaanishi jambo hilo. Inamaanisha hivi." Naye akaamini. Aliamini. Hilo lilivunja umoja, lililovunja ushirika, lililovunja muungano, lililovunja ulimwengu, lililovunja uhai, lililovunja kila kitu!

Na mtu asiyeamini Neno moja la Neno la Mungu, linavunja ushirika wote na yote. Sawa! Tunaliamini ama hatuliamini. Hebu na tudumu Nalo! Mungu alisema hivyo, na hebu tudumu Nalo. Mambo mengi ninayopaswa kuruka hapa, maana tayari wakati umepita.

104 Kama vile katika nyakati zilizopita, katika nyakati zilizopita wakati mwanadamu alipofanya jambo hili, ilileta hukumu ya Mungu ulimwenguni. Mnara wa Babeli, ule muungano wa watoto wa Kaini na watoto wa Sethi, ulileta hukumu. Daima huleta hukumu ya Mungu ulimwenguni. Unaona? Loo, umoja wa kweli pamoja Naye utainuka katika hukumu, juu yake, kama vile Nuhu alivyofanya katika hukumu hiyo pamoja na jamaa yake. Nuhu mwenye haki na jamaa yake walivuka hukumu. Walifanya nini? Walienda!

Ndugu Lee Vayle, kama ukishikilia hili, hili hapa. Hilo ndilo swali pekee ambalo hatukubaliani, yeye anaamini Kanisa litapitia hukumuni. Sioni jambo hilo. Siamini jambo hilo.

Nuhu hakupitia hukumu yo yote, alipita juu ya hukumu. Ibrahimu kamwe hakuwa na moto, alikuwa ametoka kwenye moto. Israeli hawakuwa katika hukumu za Israeli, walitenganishwa na moto, kutoka kwenye hukumu. Kanisa litapanda juu ya hukumu, katika sanduku la Roho Mtakatifu, limeinuliwa kutoka duniani.

105 Jambo hili la Baraza hili la Makanisa si kitu kingine ulimwenguni ila m—msukosuko wa bikira mpumbavu, kuachwa hapa duniani kwa ajili ya kumchagua mpinga -Kristo. Lakini Kanisa halisi la Mungu litaelea kama alivyofanya mzee Nuhu, na kuingia Utukufuni hakika tu kama ninavyosimama hapa. Hiyo ndiyo sababu Yeye anawakusanya pamoja. Hivyo ndivyo Sauti inavyonena kwenda mbele leo. Hivyo ndivyo Mungu anavyofanya, ni kukusanya mmoja kutoka Los Angeles, na mmoja kutoka Philadelphia, na mmoja kutoka Georgia, na kadhalika. Akiwakusanya pamoja, watu Wake walio tayari kuliamini Neno la Mungu aliye hai. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu, ambamo wachache waliokolewa, wachache tu." Vema, safina yetu ya Roho Mtakatifu itaelea moja kwa moja juu ya hukumu za Mungu, maana tayari tumehukumiwa, tunapomkiri Yesu, Naye alichukua hukumu yetu.

106 Madhehebu haya, hata hivyo, yana ukaidi sana! Wao ni kama Hawa, alitaka hekima yake bila kujali Neno la Mungu lilikuwa nini. Nimrodi alitaka mnara wake, haidhuru, Maandiko ama la! Walikuwa wakaidi! Hawa alijua vizuri zaidi. Sethi alijua vema kuliko kuwaangukia hao wanawake warembo. Israeli walijua vema kuliko kwenda huko nje katika uzinzi huo. Na wewe pia! Lakini wengine ni wakaidi sana, Maandiko ama si Maandiko! "Mungu atukuzwe, mama yangu alikuwa Mpresbiteri! Nitakuwa, pia." Endelea, endelea ndilo jambo pekee unaloweza kufanya basi. Mungu na airehemu nafsi yako yenye dhambi. Utaliepukaje, wakati unajua ni kweli? Na kama ukiliona Neno la Mungu, na bado hufikiri ni Kweli, basi kuna kasoro fulani katika upambanuzi wako wa kiroho. Hiyo ni kweli kabisa. Angalia kote nchini uone ambapo mambo haya yanatukia. Tuko katika wakati wa mwisho, enyi marafiki. Je! Tumepitia tu katika Nyakati za Kanisa na kujua kitakachotukia katika wakati wa Kanisa la Laodikia? Hivi hatujapitia hayo tu? Mnaona ninalomaanisha? Tuko katika wakati wa mwisho.

107 Mungu anawakusanya Wateule kutoka pepo nne za dunia. Yeye alisema angewatuma malaika na kuwakusanya. Hiyo ni kweli? Wakusanye pamoja, watenganishe na magugu. Amina. Magugu yatateketezwa, si ngano. Sawa.

Lakini, wao ni wagumu sana, watakuwa nayo ama la, haileti tofauti yoyote. Loo!

Lakini Wateule wa Mungu wanaamriwa kutoka miongoni mwao. "Jitengeni," asema Mungu, "nami nitawapokea. Msiguse vitu vyao vya kilimwengu, nami nitakuwa Baba kwenu, ama Mungu, nanyi mtakuwa wana na binti Zangu. Usijifunge nira pamoja na wasioamini, bali mtoke katika hilo!" Mungu anataka

kujitenga na ulimwengu. Anataka kuunganishwa pamoja nawe, Yeye Mwenyewe. Wala hakuna mpango wa kujibunia wa mashirika, madhehebu, wala nadharia zozote za kujibunia zitakazosimama. Itahitaji Mungu, Roho Mtakatifu, ndani yako, kukuunganisha na Mungu. Na unajuaje una Hilo? Roho Mtakatifu aliyeandika Neno atashuhudia pamoja na kila Neno; na mambo yale yale ambayo Roho Mtakatifu alifanya katika Agano la Kale, Yeye atafanya katika Agano Jipya; atafanya sasa vile vile, kwa sababu Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe hujafungwa nira na madhehebu na ulimwengu. Hufungwi nira pamoja nao. Usijifunge nira pamoja nao, bali tokeni kati yao! Ninyi mmefungiwa nira kwa Kristo. Amina. Amefungwa nira kwa Bwana Yesu Kristo.

108 Biblia inasema, katika siku za mwisho kutakuwako na makanisa, mnara mwingine wa Babeli. Wangekuwa na mfano wa utauwa, na kulikana Neno la Mungu na Nguvu, Nguvu za Neno Lake. Na Neno ni nini? Ufalme wa Mungu ni nini? Hatuna budi kuwa wa Ufalme kabla hatujakuwa raia wa Mfalme. Ni wangapi wanaojua jambo hilo, semeni "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Vema, unaingiaje katika Ufalme? Ufalme wa Mungu ni Neno la Mungu lililofanyika tena katika nguvu. Amina. Alifanya nguvu; kuondoa dhambi, kutoa ishara. Ni ishara ya namna gani? Kama ni Neno lile lile lililomtoa Musa, litaleta ishara ile ile.

Jambo lile lile lililomtenganisha Lutu vuguvugu. Sasa, tunajua Lutu alikuwa vuguvugu, na Yesu alisema hiyo itakuwa ndiyo ishara ya wakati wa mwisho. Lutu aliyevuguvugu akiketi kule, alikuwa wa kidini, hakika, yeye na mkewe. Nao walikuwa ni wa kila namna ya karamu, naye alikuwa meya wa jiji, na, loo, kulikuwa na mambo mengi sana yaliyokuwa yakiendelea. Alikuwa wa kidini sana. Angeweza kuwakaribisha wainjilisti na hao wote wapitie, alikuwa sawa kwa njia hiyo. Lakini, loo, ndugu, yeye hakuwa Mteule huyo.

109 Angalia kilichotukia! Kwa nini? Mungu yeye yule aliyemtenga na kumjia Ibrahimu na kumwonyesha thibitisho la kutengwa kwake … Mm! Ee Mungu! Jinsi ninavyotamani ninge—laiti ningaliweza tu kufanya jambo fulani kukufanya ulione. Mungu alimwonyesha Ibrahimu, kwamba alikuwa amejitenga, Yeye alimwonyesha udhibitisho wa hilo, ya kwamba Yeye alikuwa pamoja naye na yuko katikati yake. Naye Yesu alisema jambo lile lile litatukia katika siku za mwisho. Hakuna taifa lililokuwa Ibrahimu, yeye alikuwa katika uchache, bali Mungu alikuwa pamoja naye. Alikuwa amemtenga wakati huo. Tunapaswa kujitenga katika siku hizi za mwisho.

Na kama Mungu alimpa Musa ishara, kwa Israeli, nabii aliyetiwa mafuta, Nguzo ya Moto, alimpa Ibrahimu ishara. Yeye—Yeye aliwapa Israeli ishara. Yeye aliwapa wanafunzi ishara. Ishara ile ile, kila wakati! Ishara ile ile, Nguzo ya Moto!

Paulo, wakati alipokuwa njiani akienda zake Dameski, kukaangaza Nguzo ya Moto mbele yake, ambayo hata ilimtoa macho, ikampiga magotini. Hakuna mtu mwingine aliyeiona. Kila mtu akisimama pale, hawakuiona. Na Sauti ikasema, "Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "Bwana, U nani Wewe?"

Akasema, "Mimi ni Yesu." Ishara! Naye alikuwa nini? Mtume kwa Mataifa. Amina.

110 Hapa tuko katika wakati wa mwisho, tukitoka Mashariki na Magharibi, Kaskazini na Kusini. Tunafanya nini? Kujitayarisha kwa ajili ya Kunyakuliwa huko. Kujitayarisha kwa … Kushikilia wenyewe imara kwa dakika chache mpaka kila uzi umejazwa na Roho Mtakatifu. Ndipo atapanda juu. Loo, jamani! Akiwakusanya watu Wake pamoja Kwake, katika umoja wa kweli pamoja Naye, kwa sababu ni Roho Wake mmoja Mtakatifu. "Kwa Roho mmoja sisi sote tulibatizwa katika Mwili mmoja, kwa pamoja Mwili wa Yesu Kristo." Na Yesu Kristo akiishi na Roho Wake katika miili yetu, analitumikia Kanisa na kufanya mambo yale yale aliyofanya, kama—kama ishara, kama bendera kwa ulimwengu, ya kwamba tuko katika siku za mwisho, tukiwa tayari kwa ajili ya Kunyakuliwa. Loo, ninampenda, sivyo?

111 Nina kitabu hapa bado, lakini siwezi kukiendea tena, tunachelewa sana. Huenda nikakichukua wakati mwingine.

Tuko katika mwisho. Umoja. Je! Ninyi mmekuwa mmoja pamoja na Mungu? Hivyo ndivyo itakubidi kuwa. Naam. Itatubidi kuwa mmoja pamoja Naye mpaka … Hebu nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yako. Ndipo Kristo, nia Yake Mwenyewe ndani yako atatambua kila Neno aliloandika. Ilifanya hivyo katika mitume, kwa usahihi ikigawanya Maandiko, ambayo ni Kweli, unaona, Roho Mtakatifu. Kama ni Kweli, basi Yeye atashuhudia kwa kuleta ishara ile ile aliyompa Musa, ishara ile ile aliyompa Ibrahimu, ishara ile ile aliyofanya kwa Kristo, ishara ile ile aliyoifanya kwa Paulo. Tuko katika wakati wa mwisho. Yeye alisema ya kwamba hilo lingekuwa. Tuko katika wakati wa mwisho. Kanisa, kwa pamoja, linakusanyika katika umoja, mmoja hapa na mmoja pale, linajiunda.

Yeye alisema, "Kutakuwa na wawili shambani, nitamchukua mmoja." Moja. Angalia, "Wawili shambani," hiyo ni wakati wa mchana, mavuno, "Nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja. Kutakuwako na wawili kitandani," upande ule mwingine wa ulimwengu,"Nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja," wakati wa

kuja kwa Mwana wa Adamu. Na imekaribia sana, imekaribia sana.

112 Usifanye hivyo! Usifanye hivyo, Adamu! Adamu! Hawa, Adamu, hebu nikulilie, usisikilize uongo wa ibilisi tena. Dumu na Neno la Mungu, ni BWANA ASEMA HIVI. Dumu na Neno Lake. Kujitenga Nayo ni kuvunja ushirika wako na Mungu, umoja wa Mungu kwa Roho Mtakatifu. Basi kama ukisema una Roho Mtakatifu na haukubaliani na Neno, basi wewe si umoja na Mungu.

Huu ni umoja wa Mungu, wakati wewe … ile—roho uliyo nayo inakubaliana na Neno hili, na inadhihirisha Neno hili na kulifanya Neno hili nguvu kutenda kama vile lilivyofanya pale.

Hebu tuseme jambo hilo pamoja. Umoja [Kusanyiko linasema, "Umoja" —Mh.] Pamoja na Mungu ["pamoja na Mungu"] ni kuwa na ["ni kuwa na"] Roho wa Mungu ["Roho wa Mungu"] ndani yako ["ndani yako"] kukubaliana ["kukubali Pamoja na Neno ["pamoja na Neno"], Neno lote ["Neno lote"], Neno lote ["Neno lote"], na kulifanya ["na kulifanya"] kudhihirishwa ["Imedhihirishwa"] katika nguvu ["katika nguvu"].

Haya basi, huo ni umoja na Mungu. Wakati nguvu hizo zinapofanya kazi ndani yangu, zikifanya kazi ndani yako, sisi ni mmoja. Amina! Ndugu Kidd, wakati nguvu za Roho Mtakatifu ndani yangu zinapofanya kazi ndani yako, hakuna kutokukubaliana, Neno liko pale. Inatenda kazi. Amina. Inalifanya jinsi lilivyo, Mungu alifanyika mwili ndani yako kwa Neno Lake. Neno lilifanya nguvu miongoni mwenu, kila Neno!

113 Sasa, kumbukeni, Ibilisi huchukua Neno hilo lote, karibu asilimia tisini na tisa na tisini na tisa ya Hilo. Asilimia tisini na tisa na tisini na tisa ya hiyo mia, atalifanya vizuri kabisa, lakini basi ataruka hapa, na huyo ndiye anayesababisha mauti papo hapo. Hilo linavunja mnyororo moja kwa moja katikati, unaenda chini.

Kila Neno! Yesu alisema nini? "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno!" Hataishi kwa Maneno machache ya Mungu, si kwa asilimia tisini na tisa na tisini na tisa ya Neno la Mungu. Lakini kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, mwanadamu ataishi kwa Hilo.

Shetani alimchukua akampeleka kule juu na kusema, "Imeandikwa!" Unaona, kama tu vile alivyomwambia Hawa, "Imeandikwa! Imeandikwa!"

Yesu alisema, "Na pia imeandikwa …"

Yeye alisema, "Imeandikwa, 'Atawapa Malaika mamlaka juu Yako.' Biblia ilisema hivyo!" Jamani, yeye ni msomi. "Imeandikwa, 'Atawaagiza Malaika Zake wakulinde Usije ukajikwaa mguu Wako juu ya jiwe, na kukubeba.'"

Yeye alisema, "Imeandikwa pia, 'Usimjaribu Bwana Mungu Wako.'"

114 Walisema, "Tuna Maandiko," Matendo 19, "tumebatizwa na Yohana."

Paulo alikuwa na jambo lingine, alisema, "Hilo halitumiki tena." Unaona? "Yohana alibatiza tu …" Yeye hakuliamini neno la Yohana. Yeye alisema, "Nitawaambia yale Yohana aliyosema. Yohana alisema alibatiza kwa toba, si kwa ondoleo la dhambi." Dhabihu haikuwa imeuawa, unaona. Yeye alisema, "Yeye alibatiza kwa toba, akisema mnapaswa kumwamini Yeye atakayekuja." Nao waliposikia jambo hili, walibatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Paulo aliweka mikono yake juu yao iliyojaa sana Neno, na Roho Mtakatifu akaja juu yao. Walianza kutabiri, kunena kwa lugha, kumtukuza Mungu, na ni wakati ulioje! Loo, jamani. Lilikuwa ni kanisa kubwa jinsi gani? Kumi na mbili. Naam. Loo, Mungu hashughuliki kwa wingi, Yeye hutenda kazi katika mioyo minyofu. Hebu na tuwe na moyo wa namna hiyo. Je! Mnampenda? Hebu na tuombe.

115 Loo, ewe mtangaji wangu mpendwa, umewaangalia binti za Moabu au umewaona binti (ninazungumza juu ya makanisa) wa Kaini? Jinsi wanavyopotea mbali na Neno! Je, wewe, rafiki yangu wa thamani, umeona katika siku za mwisho ya kwamba mambo haya yametimia? Je! Mmekuwa mkiona hivi majuzi kuhusu namna Neno la Mungu linavyodhihirishwa? Jinsi ambavyo ufufuo uliotokea wakati mmoja umetulia, hakuna mengi yaliyosalia? Ni kitu gani? Ni utulivu kabla ya tufani. Hukumu ziko tayari. Je, mmekuwa mkiashiria mambo haya? Je! Mmelinganisha Maandiko na Maandiko, Neno la Biblia na Neno la Biblia, ushahidi na ushahidi? Je! Mmelilinganisha Neno la Yesu ambalo Yeye alisema ya kwamba ibilisi katika siku za mwisho … lingekuwa karibu sana, kama jambo halisi, hata kama angaliweza angemdanganya kila mtu isipokuwa Mteule, Mteule. Wazia tu, hilo fundisho la Kimaandiko litakuwa karibu sana! "Loo, tunamwamini Roho Mtakatifu, Mungu atukuzwe milele! Tuna Roho Mtakatifu, tunanena kwa lugha." Na halafu tugeuke na kulikana Neno? Naam. Mnaona, atawadanganya walio Wateule kama yamkini.

116 Kama kuna mtu hapa ndani ambaye si sawa na Mungu, kama kuna mtu hapa aliye mgonjwa au anayeteseka … Kuna leso na kadhalika hapa, nitaziombea. Sijali una haja gani. Kila ahadi katika Kitabu hiki ni yako. Ni yako.

Sasa, nimewaletea Neno, nimelileta kutoka Mwanzo moja kwa moja hadi siku hii tunayoishi, nikipiga

tu mahali na kuwaonyesha. Mamia mengi ya mahali ningaliweza kufikia mbali na hayo, sina wakati. Lakini hakika, katika jambo hilo, unaweza kuona ya kwamba mambo haya ya kimadhehebu yako nje. Ni dhana ya uongo ya ibilisi, wakijaribu kumpanga mtu pamoja na umoja wa nia zao na mawazo yao. Wakati, ni Roho Mtakatifu ambaye tumeunganishwa na Mungu kama mmoja. Na Roho Mtakatifu anakubaliana na Neno la Mungu. Unaona, Biblia ilisema, Yesu alisema hata wangekiri jambo hilo, unaona, "Kuwadanganya walio wateule kama yamkini." Mnaona mahali tunaposimama?

117 Sasa chukua Neno hili la Mungu katika mkono huo wa imani. Unahitaji nini asubuhi hii? Unahitaji ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo? Kidimbwi kimefunguliwa. Unahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu? Yeye anajaribu kupigana kuingia ndani yako. Unahitaji uponyaji? Mbona, Roho Mtakatifu Mwenyewe Mwenyewe, Neno ambalo limefanywa nguvu, liko papa hapa sasa, nguvu zile zile za upambanuzi zikiangalia kwenye kusanyiko hili hapa sasa na kuona ile Nuru ikizunguka -zunguka kama kumeka. Je! Nimewahi kuwaambia jambo lolote la makosa? [Kusanyiko linasema, "La." - Mh.] Nimewahi?

Kama—kama vile nabii alivyowaambia Israeli kabla hawajampata mfalme aliyetokana na binadamu, yeye alisema, "Je! Nimewahi kuwaambia lo lote … Je! Nimewahi kuchukua pesa zenu? Je! Nimewahi kuja huku na kuwasihi nipate pesa na—na kupanda magari na kuishi katika majumba makubwa makubwa ya kifalme na kujenga mambo makubwa sana na kuwanyang'anya pesa zenu? Je! Nimewahi kuwaomba hata senti moja? "Kamwe."

Je! Nimewahi kuwaambia jambo lo lote katika Jina la Bwana ila lile Mungu alilotimiza? Je! Nimewahi kunena katika Jina Lake ila jinsi ilivyokuwa? Je! Nimewahi kuwaambia ono juu ya wasikilizaji ila hasa mtu yule aliyeinuliwa, mgeni ama ye yote yule, ila yale aliyosema "Hiyo ni kweli"? Je! Nimewahi kuwaambia jambo lolote la makosa? [Kusanyiko linasema, "La." - Mh.] Basi hebu niwaambie sasa, BWANA ASEMA HIVI, mpokeeni Roho Mtakatifu, Roho atakayelichukua Neno la Mungu mikononi mwao wa imani, aende nje huko. Ufalme wote ni wako. Ni yenu, enyi watoto.

118 Kwa nini unatoka Georgia, kutoka kote nchini, kutoka Ohio, kutoka Kansas, kila mahali, kwa ajili ya mkutano mdogo? Nafikiri kanda imezimwa sasa, kwa hiyo, naweza kusema jambo hili. Unaona? Kwa nini kuja namna hii? Ni kitu gani kinachokufanya ufanye hivyo? Ni kitu gani? Ninaona watu hapa kutoka Arkansas, kutoka mamia ya maili mbali.

Jana usiku, nikija moja kwa moja kutoka Jiji la Kansas, ndugu mdogo wa Kipolishi aliyesimama kule nyuma, akaja, akaongozwa, akasema, "Ndugu Branham, tangu niliposikia habari zako kwa mara ya kwanza huko Canada miaka mingi iliyopita, mambo ambayo umeona na kutenda, nimeyachunguza moja kwa moja, moja kwa moja na mbele, juu na chini," na kusema,"hakuna hata moja lililopata kukosea." Labda yeye ni Mkatoliki wa Kipolishi, na huyu hapa anakuja, akichukua kanda, akitoka na kuzicheza, akikabiliana na upinzani. Wahudumu wanaopaswa kuwa pamoja nami na kutusaidia, lakini wakikana Nguvu zake, wakikana Kweli ya Neno, na wakidai kuwa na Roho Mtakatifu.

Sijajiita nabii. Mmefanya hivyo. Lakini, kama ndivyo ilivyo, basi Neno la Bwana linatoka wapi? Tunajuaje kama ni kweli ama si kweli isipokuwa kuwe na kitu cha kuliunga mkono? Hilo ni Neno la Mungu hapa, Neno lililoandikwa. Na halafu kama Neno lililoandikwa limeungwa mkono, basi ni Mungu katika Neno hilo akilifanya Neno hilo kuwa kweli. Paulo alisema, "Nifuateni, kama ninavyomfuata Kristo."

119 Sasa, kama una haja ya Mungu kwa ajili ya magonjwa, kwa ajili ya wokovu, nini … ama kuondoa … Baadhi yenu wanawake ambao hamjapata neema ya kutosha kuziacha nywele zenu zikue, baadhi yenu wanaume ambao hamjapata neema ya kutosha kuacha kuvuta sigara, baadhi yenu wahubiri hamjapata neema ya kutosha kukubali ukweli wa ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo, baadhi yenu wagonjwa ambao ni wagonjwa na wagonjwa kufa, mbona msichukue Neno hili asubuhi ya leo. Nitawaambia sasa, Ni mwili miongoni mwetu! Chukua Neno hilo mkononi mwako.

Hapa inaning'inia picha ukutani, ya Malaika wa Bwana, Yeye yule aliyewaongoza wana wa Israeli, Yule yule aliyekutana na Paulo, Yeye yule aliyekuwa katika Kristo. Na Roho Mtakatifu yeye yule yuko ndani yako, ndani yako, akikuunganisha kama mmoja. Ni kitu gani kinachofanya mioyo yetu ikusanyike pamoja kwa mamia ya maili? Hakuna kitu kama hicho nchini. Wanakuja kwenye Neno.

120 "Kuna chemchemi iliyojaa Damu, inayotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wasioamini hutumbukia chini ya mafuriko, na kupoteza doa lao la hatia. Tangu wakati huo kwa imani nilipoona huo mto, majeraha Yako yanayotiririka yametolewa, upendo wa ukombozi umekuwa ndio ajenda yangu, na utakuwa hivyo mpaka nitakapokufa."

121 Baba yetu wa Mbinguni, hapa kuna lundo la leso, glavu, huenda zikaenda kwa barua. Sijui ni nani aliyeziweka hapa, labda Billy, labda watu hapa katika wasikilizaji. Ninajisikia tu kufanya jambo hili sasa, Bwana. Hakuna kitu mikononi mwangu, hakuna kitu ndani yangu kama mwanadamu. Nisingeweza kutegemea ufahamu wangu mwenyewe wa kibinadamu. Sifahamu ni kwa nini jambo hili ni hivyo, bali ninafuata yale uliyosema. "Walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo, leso na nguo, na pepo wachafu wakawatoka watu." Haikuwa kwa sababu alikuwa mtu mashuhuri, ilikuwa ni kwa sababu Mungu alikuwa

pamoja naye katika Neno na nguvu. Wala kamwe hakutaka shauri kwa mitume, bali aligundua walipokutana pamoja ya kwamba Injili ile ile, ubatizo ule ule, kila kitu walichokuwa wakifanya, kilikuwa ni kitu kimoja.

122 Sasa ninaomba, Bwana, kwa ajili ya watu hawa wa thamani wanaokuamini Wewe, ya kwamba utawaponya. Hao katika wasikilizaji, waponye, Bwana. Jalia imani yao iwe juu tu na kulishika Neno hilo sasa hivi, na kusema, "Uvimbe, maradhi, maovu, afadhali uondoke, ninakata kwa Upanga wa Mungu! Ninaamini! Imani yangu ina nguvu. Ninausukuma Upanga kwa kina kirefu. Niondokeeni! Ninainuka kutoka kwenye kiti changu, niwe mzima." "Ninaweka mkono wangu juu ya baba yangu, juu ya dada yangu, mtoto wangu, juu ya jirani yangu. Ninaamini. Neno Lako ni Kweli. Mimi niko katika umoja na Wewe. Kazi ulizosema Wewe ulifanya, tungezifanya pia. Bwana Mungu, ninaamini kila Neno. Nami ninakuja mbele, nakuja mbele kulidai, kulichukua asubuhi ya leo."

123 Ee Mungu, jinsi ambavyo ningeweza kuwazia wakati kanisa lilipokuwa likiendelea, wakati Musa alipoogopa kidogo kule chini baharini, alianza kumlilia Bwana. Naye Bwana akasema, "Mbona mnanililia Mimi? Unanililia nini? Nena na usonge mbele! Sijakuagiza kufanya kazi? Nena!" Nena nini? Neno la Mungu. "Limo ndani yako. Nena na usonge mbele. Usinililie Mimi. Endelea mbele."

Na, Bwana Mungu, leo ninakuja katika Jina la Bwana Yesu. Ninakuja nikitoa Upanga huu wa imani, nikidai umoja wa Mungu na mwanadamu kwa Roho Mtakatifu, kwa rehema na dhabihu ya Yesu Kristo Mwanawe. Ninakataa kila pepo aliyemfunga mtu yeyote kwa njia yoyote katika jengo hili, kama ni mvulana au msichana, mwanamume au mwanamke. Ninakataa kila ugonjwa. Ninapinga kila shaka. Ninakataa kila hofu. Ninakataa kila kitu kisichomcha Mungu, niwaache wasikilizaji hawa katika Jina la Yesu Kristo! Tokeni kwenye wasikilizaji hawa, ili tuweze kuwa mmoja na Mungu na tuweze kumtumikia Mungu bila magonjwa wala hofu. Jalia nguvu zilizotufanya mmoja na Mungu … Shetani huyo anawezaje kuwika kote na wapakwa mafuta? Ibilisi huyo anawezaje kusimama huko nje na kuwika kama Goliathi? Wakati Daudi alipoingia kambini, na kusema, "Unamaanisha kumruhusu yule Mfilisti asiyetahiriwa asimame pale na kudhiaki majeshi ya Mungu aliye hai?"

Ee Mungu, fanya mwanaume na wanawake wainuke katika nguvu za Roho. Jalia huyo asiyeongoka, huyo ibilisi aliyehuzunika ambaye amedhuru jamii ya binadamu kote katika nyakati, asimame hapa na kulidhiaki kanisa la Mungu aliye hai? Shetani, njoo, na uondoke, katika Jina la Yesu Kristo!

124 Sasa, ninyi mlio na nguvu za kutosha kutoa Upanga, sasa kwa kuwa mna ufahamu wa kutosha katika Neno la Mungu kudai kwamba ni mali yenu binafsi, mnaoweza kuchukua Neno la Mungu sasa mkononi mwenu, kulishikilia katika mkono wa imani, na kusema, "Ninachukua upande wangu pamoja na Bwana. Nitakuwa umoja na Mungu wangu, tangu sasa na kuendelea. Nitatoa Upanga huu wa Roho katika Neno hili, nami nitamkata Ibilisi kwa kila ahadi ambayo Mungu aliniahidi."

Kama unaamini jambo hilo kwa moyo wako wote, ninakuomba basi kwa uaminifu kwa moyo wangu wote, katika Jina la Yesu Kristo, simama kwa miguu yako na ulikubali. Unamaanisha jambo hilo? Je, wewe ni mwaminifu? Neno liko mkononi mwako? Je! Mkono wako ni imani yako? Inua mkono wako wa kimwili kwa Mungu, useme, "Mungu, kwa hili, kwa mkono wangu ulioinuliwa ninaahidi maisha yangu yote. Ninaahidi nafsi yangu, ninaahidi mawazo yangu, ninaahidi kila kitu kwa Neno la Mungu. Jalia Roho Mtakatifu achukue imani yangu sasa na anipe jambo hilo. Kata kila shaka mbali nami. Na, kwa imani, ninapokea ahadi ninayoomba, wakati huu."

Kama unaamini, sema, "Amina," sasa. [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Sema, "Amina," tena. ["Amina."] Amina, amina, amina! Basi, kama unamaanisha jambo hilo kwa moyo wako wote, katika Jina la Yesu Kristo, ninakuahidi kile ulichoomba. Amina. Unaamini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki.

Ndugu Neville.

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info